SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 274,002,680
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mwinyi** atoa fursa madhehebu Bohora kuwekeza Zanzibar

UKURASA 3



**SEHEMU 8 AMBAZO NEYMAR ANAWEZA KWENDA KWA MKOPO**

UKURASA 12

Nipashe
Jumatatu Julai 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580996
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# TUCTA, waajiri wavunja ukimya kikokotoo kipya

UKURASA 2



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akitoa mada kwa wabunge mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, kwa ajili ya kuwajengea uelewa kuhusu kanuni mpya za mafao, zilizoanza kutumika Julai 1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtuhumiwa ubakaji awatoroka askari akipelekwa polisi

UKURASA 3

## Saba wapoteza maisha gari likigonga mkokoteni

UKURASA 2

MICHEZO MANARA KIKAANGONI TFF UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Mwezeshaji wa mafunzo ya tathmini ya utekelezaji kazi za jamii zenye kupinga ukatili wa kingono katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, Michael Ntibikema, akitoa mwongozo kuhusu watoa maamuzi watakaoshiriki mjadala wa sera utakaofanyika hivi karibuni, chini ya usimamizi wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO na Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Haki za Binadamu (Equtas). **PICHA: GODFREY MUSHI**

# TUCTA, ATE wavunja ukimya kikokotoo

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) na Chama cha Waajiri (ATE), vimevunja ukimya kwa kusema vimeshiriki hatua zote za kuandaa kanuni mpya za mafao ya uzeeni.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, wakati wa semina ya wabunge kuhusu uelewa wa kanuni mpya ya mafao iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako na kufunguliwa na Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu.

"Mheshimiwa Naibu Spika kwa upande wangu naomba nizungumze machache na haya yataelekea kwenye kukanusha uvumi kuwa hatukushirikishwa wakati wa kuandaa kanuni mpya ya mafao, jambo hili sio kweli nawaomba Watanzania wapuuze uvumi huo, wafanyakazi kwa maana ya TUCTA tulishiriki hatua zote," alisema Nyamhokya, Rais wa TUCTA.

Kauli hiyo pia iliungwa mkono na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzzane Ndomba, ambaye alisema kanuni mpya ya mafao iliyoanza kutumika tarehe Julai 1, 2022 ilishirikisha wadau wote kwa maana ya ATE, TUCTA na serikali.

Alisema yapo maneno ambayo yanasemwa kuwa viongozi wa wafanyakazi hawakushiriki kwenye mchakato wa kikokotoo jambo ambalo sio kweli kwa kuwa safari ya kuelekea kikokotoo ilianza mwaka 2017 na kipindi hicho hawakukubaliana, lakini kanuni hiyo viongozi wa wafanyakazi walishiriki katika hatua zote za kuandaa kanuni mpya za mafao kwenye kamati zote zilizoundwa.

"Nitakuwa mnafiki kama nitafika hapa au mahala pengine popote niende nikatamke kuwa wafanyakazi hatukushirikishwa, tumeshiriki vilivyo," alisisitiza Nyamhokya.

Akifafanua, alisema Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kulindwa na Sheria za nchi, kuna kanuni za ILO zinawabana viongozi wa vyama vya wafanyakazi kuilinda Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iendelee kuwapo wanapo kwenda kwenye vikao vya ILO.

Aliwahakikishia wabunge, wafanyakazi na Watanzania kuwa katika kuandaa kanuni mpya ya mafao, sauti za viongozi wa vyama vya wafanyakazi zilisikilizwa na ndiyo waliomba kanuni hiyo irudi kwenye asilimia 33.

Kwa upande wake, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzzane Ndomba, alisema kanuni mpya ya mafao ni bora na hawana sababu ya kuikataa kwa kuwa ilishirikisha wadau wote.

Naye Naibu Spika Zungu aliwaeleza wabunge kuwa wadau ambao ni wafanyakazi na waajiri wameridhika na kanuni hiyo na kazi kubwa iliyopo mbele yao ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu kanuni mpya ya mafao.

Awali, Profesa Ndalichako alisema uandaaji wa kanuni mpya ya mafao ambayo imeanza kutumika rasmi Julai 1, 2022 ilishirikisha wadau wa Utatu ambao ni TUCTA, ATE na Serikali.


DERM group

NOTICE

CHANGE OF NAME

Notice is hereby given that **DERM ELECTRICS (T) LIMITED** with registration number: 33548 has changed its name to:

DERM GROUP (T) LTD

The change of name has no effect in shareholding or management of the company.

Pursuant to this change henceforth, all our ongoing activities and/ or arrangements shall be in the new name.

Derm Plaza, 15th Floor, Plot 18 Block 45A, Kijitonyama, New Bagamoyo Road, P. O. Box 4756, Dar es salaam.

(+255) 22 277 4507 info@derm.co.tz www.derm.co.tz

21929601


## Saba wapoteza maisha ajali ya gari kugonga mkokoteni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATU saba wamefariki dunia na wengine watano kujeruhiwa baada ya gari kugonga mkokoteni uliokuwa ukivutwa na ng'ombe ukiwa umebeba watu 12.

Ajali hiyo imetokea kwenye Kijiji cha Lugala, Wilaya ya Chamwino, mkoani hapo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana na chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva wa gari aina ya Toyota Landcruiser lenye namba za usajili STL 9534 ambalo ni mali ya Idara ya Maji, Mkoa wa Katavi.

Alisema gari hilo lilikuwa likiendeshwa na Paschal Paulo (29), mkazi wa Katavi na ilikuwa ikitokea Dodoma kuelekea Mtera na kugonga mkokoteni huo.

"Chanzo cha ajali ni mwendokasi wa dereva wa gari, alikuwa akiendesha kwa kasi na kumsababishia kushindwa kung'amua kwa haraka kama kuna mkokoteni mbele yake," alisema.

Kamanda alisema: "Kwa sababu muda huo wa alfajiri eneo hilo huwa lina ukungu, na dereva alikuwa kwenye mwendo uelekeo sawasawa na huo wa mkokoteni ambao ulikuwa ukielekea Iringa akaugonga na watu saba walifariki papo hapo na ng'ombe wawili nao wakafa."

Kamanda Otieno alisema dereva wa gari hilo anashikiliwa kwa ajili ya taratibu za kisheria.

Akizungumza kuhusu ajali hiyo, Diwani wa Kata ya Manzase wilayani humo, John Mika, alisema mkokoteni huo ulikuwa umebeba watu 12 waliokuwa wakienda kwenye mlima wa Lugala, kuchimba udongo wanaotumia kufinyanga vyungu.

Alisema gari hilo liliugonga mkokoteni huo na kusababisha vifo vya watu saba papo hapo na ng'ombe wawili waliokuwa wakivuta mkokoteni huo.

"Majeruhi wengine wamekimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma," alisema.

Kadhalika, diwani huyo alifafanua kuwa ni kawaida kwa wanakijiji kwenda milimani asubuhi kwa ajili ya kuchimba udongo wa kufinyanga vyungu na bidhaa mbalimbali za ufinyanzi kama sehemu yao ya kujipatia kipato.

**MAJERUHI AELEZA**

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ernest Ibenzi, alisema walipokelewa majeruhi sita, lakini mmoja alifariki dunia njiani wakati akikimbizwa hospitalini hapo.

Alisema majeruhi mmoja ameruhusiwa na wengine bado wanaendelea na matibabu.

Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, Jonas Cherehani, alisema alitoka alfajiri akapanda mkokoteni huo kwa ajili ya kwenda mlimani kuchimba udongo.

Alisema hakumbuki kilichotokea kwenye ajali hiyo kwa kuwa amezinduka akajikuta hospitalini hapo.

## HABARI KITAIFA

# Mtuhumiwa ubakaji awatoroka askari polisi akipelekwa kituoni

**Na Beatrice Shayo**

MTUHUMIWA wa ubakaji mwanafunzi wa shule ya sekondari, amedaiwa kutoroka mikononi mwa askari wakati alipokamatwa kwa ajili ya kupelekwa kituo cha polisi.

Mwanafunzi aliyefanyiwa kitendo hicho (jina linahifadhiwa), alidai kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa na kupandishwa kwenye usafiri wa bajaji kuelekea kituo cha polisi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa upelelezi unaendelea vizuri.

Akisimulia mkasa huo, mwanafunzi huyo (16) alisema alifanyiwa kitendo hicho Juni 3, mwaka huu, majira ya mchana wakati akielekea kwenye msiba wa mwanafunzi mwenzake aliyefiwa na baba yake.

Alisema wakati akitoka shuleni na wanafunzi wenzake watano, walifika eneo la Karimchungwa huko Chamazi na kukutana na vijana wanne wanafunzi wa shule jirani na ya kwao.

Alisema wenzake wanne walikuwa wametangulia, yeye na wanafunzi wengine walibaki na mmoja wa vijana hao, alimshika mkono na kumvutia kichakani.

"Nilipiga kelele ya kuomba msaada lakini yule kijana alinitolea kisu. Nikakaa chini wakaniburuza na kunifikisha kichakani."

Wakati hayo yakitendeka, wanafunzi wenzake walipiga kelele za kuomba msaada, lakini hapakuwapo na mtu yeyote eneo hilo na kukosa msaada.

Alisema miongoni mwa wanafunzi wenzake, mmoja ni skauti ambaye alipuliza filimbi kutoa ishara ya hatari, lakini hawakupata msaada wowote.

Binti huyo alisema kuwa baada ya kufanyiwa kitendo hicho, kijana aliyembaka alitoka kichakani huku akikimbia.

Hata hivyo, njiani alikutana na wanaume wanne na kumkamata na kurudi naye hadi eneo alikofanya ukatili huo.

"Wale wenzangu baada ya kuona yule kijana amekamatwa na wale 'wababa', wakanibeba mpaka shule. Yule aliyenibaka akahojiwa pale shuleni na kutakiwa kuandika maelezo," alisema.

> **"Baada ya kumkosa mtuhumiwa niliwauliza askari 'nyie mnajua kosa la huyu mtuhumiwa na anatolewa kituo kidogo anapelekwa kituo kikubwa, mbona hamjamfunga pingu mpaka anakimbia?" Hawakunijibu chochote, wakaniambia tuelekee Kituo cha Polisi Maturubai,"**

**HOSPITALI**

Walimu wawili walimpeleka Hospitali ya Chamazi kwa kushirikiana na mama na dada yake, alifanyiwa vipimo na kupatiwa dawa maalum kwa waathirika wa matukio ya ubakaji.

Mama wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alisema alipigiwa simu na mwalimu kufahamishwa afike Kituo cha Polisi Chamazi, kuwa kuna tatizo dhidi ya mwanawe.

Alipofika kituoni huko, alimuona mtoto wake akiwa ameshikiliwa na mwalimu na kushtuka.

Alisema baada ya muda mfupi, askari polisi alimjulisha kuwa hapakuwapo na gari la kituoni kwa ajili ya kumsafirisha mtuhumiwa kwenda kituo kikubwa cha Polisi Maturubai.

Alisema askari walimwomba pesa alizolipwa kwa ajili ya matibabu ya binti yake na ndugu wa mtuhumiwa zitumike kukodi bajaj ya kumpeleka mtuhumiwa kituoni.

Mama alisema mmoja wa askari alikaa mbele na dereva na wawili nyuma na mtuhumiwa. Mwanawe mkubwa aliambiwa ampakate mdogo wake (mwanafunzi) kuelekea kituoni.

**MTUHUMIWA ATOROKA**

Dada wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), anasema walipofika katikati ya Kituo cha Mkongo na Kanisani, mtuhumiwa alichoropoka kwenye bajaj kwa nyuma na kukimbia.

Alisema aliwataarifu askari ambao walimfukuza bila mafanikio.

"Baada ya kumkosa mtuhumiwa niliwauliza askari 'nyie mnajua kosa la huyu mtuhumiwa na anatolewa kituo kidogo anapelekwa kituo kikubwa, mbona hamjamfunga pingu mpaka anakimbia?" Hawakunijibu chochote, wakaniambia tuelekee Kituo cha Polisi Maturubai," anasema.

Walipofika eneo linaloitwa Kwa Mbiku, mmoja wa askari hao (mwanamke) alishuka na kubaki na askari wawili.

Anasema walipofika Kituo cha Polisi Maturubai, mmoja wa askari hao alishuka na mafaili, kwenye bajaj akabaki askari mmoja.

"Nilipofika mapokezi, nikaambiwa nitoe maelezo, nikawaambia 'ninatoaje maelezo wakati mtuhumiwa amepotea mikononi mwenu?" Wakaniambia 'wewe siyo uliyefanyiwa tukio, aliyefanyiwa tukio ndiye anapaswa kutoa maelezo.'

Anasema mmoja wa askari alimtaka akanunue karatasi ya kufungulia kesi, lakini alimjibu kwamba hakuwa na fedha ya kununua, baadaye mmoja wa askari aliamua kwenda kununua.

"Nikarudi ndani ya kituo na mdogo wangu, tukaingia ndani kuhojiwa. Askari akamuuliza 'aliyekufanyia hicho kitendo unamjua?' Mdogo wangu akajibu 'simjui'. Askari akamwambia 'kama humjui, mimi nifanyaje?'

"Baada ya mahojiano, alipatiwa RB na tukaambiwa tukamtafute mtuhumiwa, tutakapomwona, turudi kutoa taarifa," anasimulia.

SHULENI

Mwalimu wa nidhamu katika shule anayosoma msichana huyo, alisema tukio hilo lilitokea Juni 3, mwaka huu majira ya saa 6:20 baada ya raia mwema kufika shuleni hapo akiwa na mtuhumiwa pamoja na wanafunzi waliokuwa mashuhuda.

"Baada ya hapo tulipiga simu polisi kumjulisha tunamshikilia mtuhumiwa na ndipo walipotuma askari jamii, huyu askari jamii alifanya mawasiliano na kumchukua mtuhumiwa kwa bodaboda kwenda Kituo cha Polisi Chamazi," anasema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Temeke alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na tukio hilo, alisema ameshangazwa na taarifa hizo na kuahidi kwenda kuzifanyia kazi na kutoa taarifa.

Nipashe iliendelea kufuatilia taarifa hizo kwa kamanda huyo zaidi ya wiki moja bila majibu na baadaye alisema yeye sio mzungumzaji, atafutwe Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro.

# Mwinyi atoa fursa madhehebu Bohora kuwekeza Zanzibar

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi amefanya mazungumzo na Kiongozi Mkuu wa Madhehebu ya Bohora duniani, Syedna Muffaddil Saifuddin na kutoa fursa kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa dhehebu hilo kuwekeza visiwani humo.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu Zanzibar, mazungumzo hayo yalifanyika Ikulu, na kiongozi huyo wa Madhehebu ya Bohora akiwa na ujumbe wake walionyesha azma ya kuendelea kumuunga mkono Rais Mwinyi katika juhudi zake za kuwaletea maendeleo wananchi wa visiwani humo. "Katika mazungumzo hayo Rais Dk. Mwinyi alimweleza kiongozi huyo fursa mbalimbali zilizoko pamoja na mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anayoiongoza katika biashara na uwekezaji," ilieleza taarifa hiyo.

Ilieleza kwamba Dk. Mwinyi pia aliwakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara wa dhehebu hilo kubwa duniani kuja kuwekeza Zanzibar na kuwahakikishia kwamba serikali imeweka mikakati madhubuti sambamba na ushirikiano mkubwa.

"Zipo fursa nyingi Zanzibar, mnakaribishwa hakika serikali imejipanga na mazingira yameboreshwa, miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na sekta ya utalii, uchumi wa buluu ambao unajumuisha matumizi na uendelezaji rasilimali za bahari.

Hii ni mara ya pili ndani ya miezi mitatu Dk. Mwinyi kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara kuwekeza visiwani humo. Aprili 22, mwaka huu, Dk. Mwinyi alifanya mazungumzo na ujumbe wa baadhi ya wawekezaji kutoka nchini Uingereza ulioongozwa na Msaidizi wa Waziri Mkuu katika masuala ya Biashara, Lord Wanley.

Ujumbe huo pia uliambatana na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar. Kwenye mazungumzo hayo, Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu, kikiwamo kilimo cha mwani na uvuvi wa bahari kuu. Alisema serikali anayoiongoza inafurahi kufanya kazi na wawekezaji katika miradi mbalimbali iliyomo katika sekta ya uchumi wa buluu.

Alitaja baadhi ya matatizo yanayokabili maeneo hayo ni ukosefu wa soko na kiwango kidogo cha bei katika zao la mwani.


## KUPOTEA KWA CHETI



**BEATUS RIZIK THOMAS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1110-0167** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KALOLENI SEKONDARI mwaka 2010.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/476871/2021.**



## BISMILLAH RAHMAN RAHIM



16928002

Familia ya marehemu **Dk. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea **Marehemu Dk. Omar Ali Juma** itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **7 Julai, 2022 saa kumi jioni** katika **Msikiti Wa Ngazija**

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Ndugu, marafiki na jamaa wote mnakaribishwa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.**

**AMIN**




Janeth Mwamtobe mnufaika wa mpango wa msaada wa matibabu kwa watu wanaotumia dawa za kulevya unaotekelezwa na Taasisi ya Henry Jackson Medical Research International (HJFMRI) ya Mbeya na Songwe akitoa ushuhuda wake kwa Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, jinsi mpango huo ulivyobadilisha maisha yake na kuwawezesha wengine kutojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya. Waziri Mkuu alitembelea banda la maonyesho la HJFMRI katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Matumizi ya Dawa za Kulevya na Biashara Haramu. Watatu kushoto ni Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Gerald Kusay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Pinda ataka wachoraji waendelezwe

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameshauri vijana wanaojihusisha na sanaa za ufundi na uchoraji watafutiwe fursa za kujiendeleza nje ili kazi zao ziwe na ujumbe utakaouzika kwa gharama kubwa.

Agizo hilo limeungwa mkono na kundi hilo huku mmoja wao akitoa ushuhuda wa kuuza nje ya nchi kazi yake kwa Sh. milioni 10.

Agnes Mpata, mchoraji nguli kutoka kundi la Tingatinga Arts, lililopo Oysterbay mkoani Dar es Salaam, akiwa miongoni mwa mchoraji wa sanaa ya uchoraji walioshiriki maonyesho yaliyoandaliwa na Ubalozi wa India nchini, alitoa ushuhuda wa namna alivyouza picha hiyo aliyomchora mnyama chui akiwa na mtoto wake wakiwa wameshiba wakielekea kupumzika.

Katika maonyesho hayo yaliyopewa jina la 'Rhythms of India' yalihusisha pia mchoraji nguli kutoka India, Narendar Reddy na wasanii wazawa wamezungumzia fursa hiyo ni kubwa kwa kubadilishana uzoefu katika sekta hiyo na kupata masoko zaidi nje ya mipaka ya Tanzania.

Akifungua maonyesho hayo juzi yaliyofanyika ubalozi wa India, Pinda alisema moja ya mambo yaliyomvutia katika biashara ya picha siku hiyo ni vijana wa Tanzania kushirikishwa katika maonyesho hayo yaliyomhusisha msanii mkubwa wa uchoraji kutoka India.

Alisema kupitia maonyesho hayo, waendelee kuiomba Serikali Tanzania na India waone namna gani wanaweza kuiendeleza ili wapate vijana watakaokwenda kusoma na kujifunza zaidi kwao.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan ambaye eneo la uwekezaji amelipa nafasi kubwa na msisitizo kwa Watanzania ni kukaa mkao wa kuona ni namna gani watanufaika kutokana na wawekezaji wanaokuja kuwekeza Tanzania.

Mchoraji Agnes alisema fursa aliyopata ya kushiriki maonyesho hayo ni muhimu kwake kujitangaza na kuuza bidhaa zake za sanaa kwa sababu ni adimu kuipata huku wateja wao wengi wakiwa ni wageni ambao hawajui walipo.

"Hapa nimekuja na picha ya mnyama tembo ambao wanapatikana Tanzania, picha hii ni ya kutoa ujumbe kwa wananchi wawahifadhi, wasiwang'oe meno tuzidi kuwatunza kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo na tumuunge mkono Rais Samia kupitia filamu ya The Royal Tour. Tunamshukuru sana Balozi wa India kwa kutupa fursa hii ya kutangaza kazi zetu kimataifa," alisema.

Alisema fursa ya kuongeza elimu nje ya nchi ni muhimu kwao kwa sababu ndiyo namna ya kupata maarifa mapya na kujua wageni wanataka nini ili wakidhi matakwa yao na wao kujiongezea kipato.

Zainab Songora kutoka Arusha alisema katika maonyesho hayo ameonyesha picha yenye mchoro wa mama akimbusu mtoto yenye ujumbe kuwa upendo wa mama hauelezeki na mtoto anapokuwa naye hujiona yupo sehemu salama.

Joshua Urio kutoka Arusha aliyeanza sanaa hiyo tangu mwaka 2018, alisema kati ya picha 100 alizochora, ameuza 40 kwa bei tofauti.

"Picha niliyokuja nayo hapa ni mchoro wa mwanamke aliyeweka mkono mmoja juu akionyesha ana nguvu licha ya utawala wa kimabavu uliopo kwa wanaume. Binafsi ninamshukuru Balozi wa India nchini, amesaidia kukuza vipaji vyetu na hii inahamasisha vijana wenzetu kufanya kazi kwa bidii, tunaomba balozi zetu zilizopo nchi mbalimbali wafanye jambo kama hili ili tutangaze kazi zetu kimataifa," alisema.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan alisema maonyesho hayo yatafanyika kwa siku tano na yalianza Jumamosi iliyopita.

"Kazi mbalimbali za wabunifu wa uchoraji wa Tanzania zilizochaguliwa na za Narendar Reddy zitaonyeshwa," alisema.

Mbunifu wa uchoraji kutoka India, Narendar Reddy alifurahishwa na kazi zilizofanywa na Watanzania waliojitokeza katika maonyesho hayo na kueleza kuwa zina nguvu katika sekta hiyo.

Alisema wiki iliyopita alikuwa na wachoraji hao wa Tanzania katika mafunzo yaliyoandaliwa na Kituo cha Utamaduni cha Swami Vivekananda cha jijini Dar es Salaam kwa ushirikiano wa ubalozi huo na kubadilishana mawazo ya kuboresha kazi zao ili ziwe bora zaidi.

Alisema katika maonyesho hayo amevutiwa zaidi na michoro ya baadhi wachoraji ambayo inaelezea utamaduni wa Mtanzania na vivutio vya utalii kupitia picha za wanyama walizochora.

# Mkenda akemea migongano Skauti

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amekemea migongano ya viongozi wa Chama cha Skauti Tanzania.

Prof. Mkenda ambaye ni Rais wa Skauti Tanzania, aliyasema hayo juzi jijini hapo katika mkutano wa uchaguzi wa wajumbe wa bodi ya chama hicho.

Alisema katika vipindi mbalimbali vya uongozi kwa muda mrefu kumekuwa kukiibuka migogoro na chokochoko kila uongozi unapokuwa madarakani.

"Sasa leo tuhakikishe ni mara ya mwisho kwa Skauti Tanzania kupata mafua, kitakachofanyika leo (jana) kifungue ukurasa mpya, mambo makubwa yaliyofanywa na viongozi wetu wa nyuma na sasa haiwezi kuchafuliwa na mafua, hivyo sokomoko hilo mwisho leo," alisisitiza.

Alisema haiwezekani kuwa na Skauti ambayo kwa katiba yake imemweka Rais kuwa mlezi halafu wafanye mchezo.

"Hatuwezi kuwa na Skauti yenye majina ya viongozi wakubwa wamekubali kuwa katika uongozi halafu tukaleta mzaha mzaha, uadilifu wa Skauti nidhamu ya lazima ionekane, ni mara ya mwisho kuwa na ugomvi kama klabu za mpira," alionya.

Waziri Mkenda alisema mgogoro huo, uliilazimu wizara kuunda kamati ya mpito iliyokuwa chini ya Skauti Mkuu, Mwantumu Mahiza ambayo ndiyo iliyoandaa mkutano wa uchaguzi.

"Mkutano huu watachaguliwa wajumbe majina matatu ya bodi ambayo yatapelekwa kwa mlezi wa Skauti Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan kumteua Skauti Mkuu," alisema.

Aliwataka viongozi waliochaguliwa wanalinda heshima na mali za Skauti, watende haki na kusimamia nidhamu na uadilifu.

Kadhalika, Prof. Mkenda aliutaka uongozi mpya wa Skauti Tanzania kuongeza kasi ya kuimarisha katika shule na vyuo ili kukabiliana na ukatili wa kijinsia na malezi.

"Kumekuwa na mambo ya ovyo kutokana na wanafunzi kukosa shughuli za kufanya kama kujiunga na Skauti, hivyo ongezeni maradufu skauti shuleni ili ipunguza ukatili wa kijinsia na kuimarisha nidhamu, maadili na uadilifu," alisema.

Naye Skauti Mkuu, Mahiza alisema chama hicho kimeweka mikakati ya kuondoa utegemezi na mpaka sasa imepata eneo jijini Dodoma kwa ajili ya kujenga kambi ya kimataifa ya Skauti, shule ya michezo, chuo cha ufundi na kitega uchumi na Rais Samia ameahidi kuwapatia fedha ya kujenga.

Awali, Askofu Mkuu, Grevas Nyaisonga, alisema wadhamini wa Skauti wamefarijika kuona chama hicho kinazidi kuwa imara kuwapo na heshima.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani wa Zanzibar, Gulamu Hussein, alisema Skauti Zanzibar iko salama na inazidi kuimarika na kustawi huku akisema tayari wameshateua majina ya wajumbe ambao wataunda timu ya kusimamia mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Chama hicho.

# Ukataji miti unavyoathiri mazingira, mifugo Pwani

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI wa Kijiji cha Chamakweza, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani wamelalamikia ukataji miti uliokithiri na kusababisha athari kwa mifugo yao ikiwamo kufa kutokana na uharibifu wa mazingira.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, wananchi hao walilalamikia kitendo cha ukataji miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na kusababisha uharibifu wa mazingira na mifugo yao kukosa chakula hali inayowalazimu kuihamisha kwenda maeneo mengine kutafuta nyasi.

Jacob Samweli, mkazi wa kijiji hicho alisema ukataji wa miti umeleta athari hasa kwa mifugo kushindwa kupita kutokana na miba mingi baada ya kuchoma mkaa kukosa maji.

"Tunaathirika na hali ya jangwa zamani kulikuwa na misitu mingi na miti mikubwa kwa sasa miti hakuna kumekuwa jangwa kutokana na mazingira hayo mifugo tumeihamisha kuipeleka maeneo mengine ili iweze kupata nyasi mwaka, jana mifugo mingi ilikufa," alilalamika.

Aidha, alisema mikaa inayochomwa inasafirishwa kulekea maeneo ya mjini bila kufuata sheria na kushauri itumike nishati mbadala ikiwamo gesi ili kulinda mazingira.

"Wanatuharibia mazingira na mwisho wa siku miti itaisha tunajikuta tunapata hasara tunashauri wasishawishi watu kuja kukata miti wajitahidi kuangalia nishati nyingine kwa ajili ya kupikia ili misitu ibaki kuwa salama na jamii nyingine iweze kufurahia uwapo wa misitu," alisema.

Alisema, wanajitahidi kutunza mazingira wanapowabaini wahalifu huwakamata na kuwakataza wasiendelee kufanya uharibifu.

"Tulikuwa na mabwawa ya asili na uoto wa asili baada ya uharibifu huo wa ukataji wa miti mabwawa yamekauka hakuna kitu kwa sasa tunachangamoto tumehamisha mifugo kwenda maeneo mengine kama Mkuranga kutafuta malisho," alisema.

Naye Lengayo Koletu alisema, athari ya ukataji wa miti ni ukame katika eneo hilo.

Alidai wanaofanya uharibifu huo hawachukuliwi hatua kali na kuwafanya kurudi bila woga.

Alisema wachungaji wanajisikia vibaya, hawapendezwi na hali hiyo na wakati mwingine wanapowakuta waharibifu hao porini huwakimbiza ili kuhakikisha mazingira yanalindwa.

Baadhi ya wanaofanya shughuli za ukataji wa miti, Kondo Mwaule, alisema wanafumbiwa macho kutokana na hali zao mbaya za maisha ingawa ni kweli wanafanya uharibifu wa mazingira. "Serikali iangalie ifanye jambo gani ili tupate kula na wengine wasiingie katika ukataji wa miti ikishindikana ujue wananchi wengi wataathirika," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mbala, Lepa Mumbi, alisema tatizo hilo limekuwa ni kero kwa sababu wanakosa vivuli vya ng'ombe kupumzika.

"Pori zima linakuwa na miba na tatizo ni huo ukataji wa miti katika kijiji tunashindwa kuwakamata kuna wakati wanakuja kukata miti usiku wakijua huo muda tumelala," alisema.

Alisema mara kwa mara wamekuwa na kikao cha kitongoji na kuwaeleza marufuku ya kukata miti ndani ya eneo hilo, lakini bado wanaendelea kwa kificho.

Mumbi alisema kitongoji chao kimeathirika kwa asilimia 60 kuanzia mwaka 2018 hadi sasa kutokana na ukataji wa miti.

Aidha, aliiomba wizara husika ifungue macho kuweka katazo mahususi kwa ajili ya kudhibiti biashara ya mkaa ili kulinda miti inayokatwa kienyeji.

# Afrika yatakiwa kuungana soko la pamoja kibiashara

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mtendaji wa Eneo huru la Biashara Afrika, Wamkele Mene, amesema Afrika haitafanikiwa kufikia ukombozi wa kibiashara endapo nchi hizo hazitakubali kuungana na kuwa na soko la pamoja.

Mene alitoa kauli hiyo jana wakati akifungua rasmi Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema bado kunahitajika nguvu kubwa ya kuleta mapinduzi ya kibiashara kwenye nchi hizo ili zizalishe bidhaa bora na kuwa huru kufanya kwenye soko la ushindani kimataifa.

"Nchi za Afrika tunahitaji kukubaliana kuwa na soko la pamoja. Si Tanzania, Kenya wala nchi yoyote itafanikiwa kupata uhuru huu kama hazitakubaliana kuwa na soko la pamoja," alisema Mene.

"Na ndiyo maana hata kunapotokea majanga kama ya milipuko ya magonjwa na vita, nchi nyingi za Afrika zinayumba kwa sababu ya kukosa uhuru wa kujitegemea kibiashara."

Alitoa mfano kwamba hata ulipoingia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 pamoja na vita vya Ukraine, uchumi wa nchi nyingi za Afrika uliyumba kwa kuwa baadhi ya bidhaa hutegemea kutoka kwenye nchi hizo.

"Ndiyo maana nasema hivi hakuna mtu yeyote atakayetoka duniani huko kuja kututafutia ukombozi kwenye eneo hili, tunahitaji kushirikiana kupambana wenyewe," alisema Mene.

Kwa upande wa Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, alisema wamemhakikishia kiongozi huyo wa soko huru la biashara Afrika kuwa wanatumia soko hilo kuuza bidhaa zenye ubora.

"Kiongozi huyu baada ya kutembelea mabanda yetu, amesema amegundua tunatengeneza bidhaa nzuri na bora, lakini shida kubwa iliyopo ni kwamba bado hatujafahamu namna ya kuchangamkia soko nje ya Tanzania na ametushauri tuziongezee thamani na tukashindane," alisema Kijaji.


TRA

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA**

**USAJILI WA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI (EFDs) KWA WAFANYABIASHARA WOTE KATIKA ENEO LA MKOA WA KODI KARIAKOO**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu wafanyabiashara wote katika eneo la mkoa wa kodi Kariakoo kuwa wanapaswa kusajiliwa na kupewa namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015. ***Wafanyabiashara wote wanatakiwa kujisajili na kupatiwa TIN*** ndani ya siku kumi na tano (15) tangu tarehe ya kuanza kwa biashara husika.

Sambamba na hatua hiyo napenda kuwajulisha ***wafanyabiashara wote katika eneo la mkoa wa Kodi Kariakoo kuwa wanatakiwa kumiliki na kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFDs)***. Maelekezo haya yanatolewa kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi na yanalenga kuboresha usimamizi wa kodi katika eneo hilo ambalo ndio kitovu kikuu cha biashara nchini.

Kuanzia tarehe ya tangazo hili, mfanyabiashara atakayeendesha biashara yoyote katika eneo la Kariakoo bila kuwa na TIN na kutumia mashine ya kieleketroniki ya kutolea risiti (EFD) atakuwa ametenda kosa kisheria linalopelekea adhabu, kifungo au vyote kwa pamoja. TRA itaendesha zoezi maalum katika eneo la Mkoa wa Kodi Kariakoo kuhakikisha kuwa sheria na taratibu za uendeshaji biashara kama ilivyoelezwa katika Tangazo hili zinafuatwa.

Wafanyabiashara wote katika eneo la Mkoa wa Kodi Kariakoo wanahimizwa pamoja na maeneo yote nchini kuendelea kuzingatia sheria na taratibu za kodi ili kujiepusha na usumbufu usio wa lazima. Uzingatiaji wa sheria na taratibu za kodi ni msingi wa kujenga jamii ya walipakodi wazalendo wenye mchango mkubwa katika makusanyo ya Mapato nchini na hivyo kuchangia kwa vitendo jitihada za Serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo endelevu.

Kwa maswali, maoni, ushauri au taarifa zaidi tafadhali usisite kutembelea ofisi ya TRA iliyopo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia: Tovuti: **www.tra.go.tz** WhatsApp: **0744 23 33 33** Namba za Bure: **0800 750075, 0800 780 078 na 0800-110 016** Barua pepe: **huduma@tra.go.tz services@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

A. J. Kidata

**Kamishna Mkuu**

21928801

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila timu imevuna ilichopanda kwa msimu huu 2021/2022

**MSIMU** wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021- 22 umemalizika rasmi juzi baada ya fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) uliowakutanisha Yanga na Coastal Union kwenye dimba la Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Yanga walitawazwa kuwa mabingwa wa FA baada ya kuifunga Coastal kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-1, huku pia wao ndio wakiwa mabingwa wa Ligi Kuu.

Kwa msimu huu kila timu ikivuna kile ilichopanda, lakini safari ya mavuno hayo ilikuwa ya kupanda na kushuka.

Simba baada ya kukosa ubingwa ilijihakikishia utawala wa nafasi ya pili na hakuna aliyekuwa akimsumbua hadi mwisho.

Presha kubwa ilianzia nafasi ya tatu hadi ya 15 na kuifanya ligi kunoga zaidi licha ya Yanga kutangaza ubingwa mapema.

Ukiacha Mbeya Kwanza ambao hawakusubiri mpaka mechi za mwisho na kushuka daraja mapema, timu nyingine zote zilizosalia zilibaki bila ya kujua hatima yao mpaka dakika 90 za michezo yao ya mwisho.

Azam ilifanikiwa kumaliza nafasi ya tatu, ambapo ilihitaji matokeo ya ushindi pekee kwenye mechi ya mwisho bila kujali hatima ya Geita Gold iliyokuwa ikimfukuzia kwa karibu, lakini kama ingepata matokeo mengine, basi leo tungekuwa tunazungumza mengine.

Azam ilifanikiwa kuifumua Biashara United kwa mabao 4-1 na Geita kutoa sare ya 1-1 na Coastal Union na hivyo kuifanya Azam imalize kwa pointi 49 dhidi ya Geita waliofikisha 46. Kwa namna hiyo, Azam imeepuka kikombe cha kumsubiri mshindi wa fainali ya Kombe la FA ili ijue hatima yake ya ushiriki ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Ni hivi, Yanga imeshakata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutwaa ubingwa wa ligi, na baada ya kuishinda Coastal maana yake, Geita iliyomaliza ya nne itakwenda Shirikisho Afrika.

Azam walionekana kupambana kumaliza nafasi ya tatu kwa udi na uvumba kiasi cha kuweka rekodi ya kuwa timu pekee msimu huu kushinda mechi nne mfululizo na sare moja katika mechi zake tano za mwisho za ligi.

Awali Azam ikiwa chini ya kocha George Lwandamina ilishindwa kusimama sawa sawa, ikitoka kwenye kuwania ubingwa na kuonekana ikitapatapa kwa matokeo yasiyoridhisha hadi ilipokabidhiwa kwa Abdihamid Moallin. Moallin alianza kwa mbwembwe za ushindi kabla ya baadaye kupunguzwa spidi lakini akachanga karata zake sawa sawa na kurejea kwenye njia iliyompeleka kwenye mafanikio ya mechi za mwisho.

Kilichotokea kwa Azam mwanzo wa ligi ndicho kilichokuwa kwa Geita ambao ndio ulikuwa msimu wao wa kwanza kushiriki Ligi Kuu Bara. Walianza vibaya chini ya Ettiene Ndayiragije, wakamfurusha na mikoba akakabidhiwa Fred Minziro aliyeipandisha Ligi Kuu timu hiyo.

Minziro aakaibeba Geita, mara ya kwanza ilieleza malengo yake ni kusalia tu kwenye ligi lakini kwa mwendo aliokuwa nao wakabadili gia angani na kukomalia kumaliza nafasi nne za juu, mwisho imewezekana.

Geita pia ndiyo imetoa mfungaji bora msimu huu, George Mpole aliyefunga mara 17 dhidi ya Fiston Mayele wa Yanga waliyekuwa wakifukuzana kuishia kufunga mabao 16.

Namungo waliomaliza chini ya Geita, wao walikuwa na mwendo mzuri lakini ghafla mambo yalibadilika kwenye mechi za mwisho na hasa baada ya mshambuliaji wao namba moja, Reliants Lusajo aliposimama kufunga na kuganda mpaka mwisho wa ligi akiwa na bao zake 10.

Hata hivyo, uwepo wa David Molinga na Shiza Kichuya kwenye timu hiyo kulisaidia kuiweka kwenye ushindani wao wa awali, lakini ikajikuta inamaliza ya tano.

Hivyo kwetu sisi Nipashe tukiwa kama wadau wakubwa wa mpira wa miguu hapa nchini, tathmini yetu tunaona kwamba, kila timu imevuna kile ilichokipanda kwenye ligi hiyo.

Hata hivyo, tunaamini huu ni wakati muafaka kwa kila timu kujitathmini na kurekebisha upungufu uliyojitokeza na kujipanga vizuri sana kwa msimu ujao wa Ligi Kuu.

Tunazitakia timu zote maandalizi mazuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Yanga, timu zijipange kusajili vizuri

**ULIKUWA** ni msimu wa kukumbukwa kwa wanachama na mashabiki wa Yanga. Wametwaa kila kitu. Ngao ya Jamii, Ubingwa wa Tanzania Bara na Kombe la FA. Kitu pekee walichopokonywa ni Kombe la Mapinduzi, ambalo lilichukuliwa na watani zao wa jadi Simba. Nao wamewanyang'anya mataji matatu, hayo niliyoyaweka mwanzo.

Kitu ambacho kilichowasaidia zaidi Yanga msimu huu ni usajili bora walioufanya kabla ya msimu kuanza. Walikuwa wakisajili huku baadhi ya watu wakiwadhihaki. Hawakujali, ligi ilipoanza ndipo mbivu na mbichi zilipojulikana.

Ikageuka kuwa moja ya timu tishio, licha ya makosa ya hapa na pale ya waamuzi, lakini ilikuwa ni timu ngumu sana na ambayo timu nyingi zilikuwa hazipendi kukutana nayo.

Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ambaye timu yao haikufungwa mechi yoyote na Yanga msimu huu, badala yake kutoa sare mara mbili, alisema msingi mkubwa au nguvu ya Yanga ilikuwa ni kwenye kiungo.

Alisema Yanga ilizishinda timu nyingi msimu huu kwenye nafasi ya kiungo, hivyo yeye alikuwa anatengeneza mpango mkakati kwa wachezaji wake kutowapa nafasi viungo wa timu hiyo kuwa huru na mpira na kuamua wafanye wanavyotaka.

Ndiyo maana Yanga msimu huu haikupata ushindi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa timu mbili tu, Simba na Mbeya City kwa kupata sare mbili, lakini zilizobaki, ama imeshinda zote mbili, au mechi moja imepata pointi tatu na nyingine sare.

Msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika rasmi kwa kushuhudia ligi ya aina yake. Ligi ilikuwa ngumu, lakini yenye maelezo. Pamoja na ugumu wake haikuwa ngumu juu, yaani kwenye timu za kusaka ubingwa.

Yanga haikuwa na timu iliyoipa changamoto huko juu, badala yake ilionekana dhahiri kuwa inakwenda kutwaa ubingwa kirahisi.

Cha ajabu Simba ambayo msimu huu imepoteza mechi nyingi na haikuwa bora, nayo ni kama ilikuwa imejimilikisha nafasi ya pili mapema. Ilifikia wakati rekodi zilionyesha hata ikifungwa mechi zote zilizobaki, basi itamaliza ya pili tu.

Kwa ligi ambayo timu zingekuwa zinashindana kwenda juu, Simba msimu huu ilistahili kuwa wa tano wa sita.

Azam ndiyo kabisa ilikuwa haivutii. Siyo Azam ile tunayoijua. Ilifanana na timu zingine kama Mbeya Kwanza, Dodoma Jiji, Coastal na nyinginezo.

Msimu huu ligi ilionekana ngumu kwa sababu nyingi zilifanana uwezo, ukiondoa Yanga na Simba.

Ndiyo maana pilikapilika ilikuwa huku chini, timu zikisaka nafasi ya tatu na ya nne, pamoja na kubaki Ligi Kuu kuliko kusaka ubingwa.

Tunakwenda msimu mwingine wa 2022/23, ambayo kwa mujibu wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), utaanza Agosti 17, mwaka huu. Ni wakati sasa wa timu zote zilizo kwenye Ligi Kuu kufanya usajili wa maana ili kupambana kuusaka ubingwa zaidi na si kupigania kushuka daraja. Timu nyingi zilisaka ubingwa ndipo ligi itanoga zaidi.

Tayari Azam imeonekana haitaki mzaha, imeanza kushusha vifaa, ikileta Waivory Coast wawili, Tape Adinho na Kipre Junior, pamoja na Mnigeria, Issa Ndala.

Inaonekana tayari imeshajua ilipokosea, hivyo imeanza kujipanga. Timu nyingine ni Simba. Nayo inakwenda kucheza Ligi ya Mabingwa. Ni timu inayotegemewa zaidi kwenye kuibeba Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa sababu imeshakuwa na uzoefu. Pia inahitaji mechi moja tu kuingia makundi tofauti na zingine.

Kwa jinsi ilivyo ni kwamba inahitaji marekebisho mkubwa zaidi kuliko timu zingine zote zinazokwenda kucheza michuano ya kimataifa.

Kuna timu zilizobaki Ligi Kuu na zile zilizopanda daraja. Zinatakiwa zitafute wachezaji bora na si bora wachezaji. Zitafute wachezaji watakaoziwezesha timu hizo kuleta ushindani mkubwa na wa kweli, si kusajili wachezaji wa bei rahisi, au waliocheza soka muda mrefu Ligi Kuu, lakini viwango vya kawaida.

Msimu ujao tunataka ligi yenye ushindani wa timu angalau tano kupambana kuusaka ubingwa.

Na hauwezi kutokea kama timu zisipofanya usajili makini na wachezaji wenye uwezo, kiu ya mafanikio, viwango na wapambanaji.

HABARI KITAIFA

# Hatimaye wapata uhakika majisafi na salama

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKAZI wa Kijiji cha Chakama Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara, hatimaye wameanza kunufaika na huduma ya majisafi na salama baada ya kijiji chao kutokuwa na huduma hiyo kwa muda wa zaidi ya miaka ya 30.

Wamempongeza mbunge wa jimbo hilo, Geofrey Mwambe kwa jitihada zake za kuwapambania na kupata majisafi na salama na serikali kukubali kuwaletea kwenye kijiji chao.

Walitoa pongezi hizo walipokuwa wakizungumza na gazeti hili wakati wakipongeza mbunge wao kuwasemea kwa serikali na sasa kijiji hicho kimejengewa tangi kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi lita zaidi ya 50,000 za maji.

Walisema kwa miaka mingi kijiji chao hakikuwa na majisafi jambo ambalo hata ufanyaji kazi za kimaendeleo ulikuwa mgumu kutokana na muda mwingi kutumika kutafuta maji.

Bakari Salumu, mkazi wa Kijiji cha Chakama, alisema kukosekana kwa huduma ya majisafi na salama kulisababisha wananchi wa kijiji hicho kutumia maji kutoka kwenye vyanzo visivyo salama.

Alisema maji hayo yalisababishia magonjwa mbalimbali yakiwamo ya tumbo.

Rehema Azizi alimpongeza mbunge wa jimbo hilo kwa jitihada zake za kuhakikisha huduma ya maji yanapatikana na hatimaye amefakinisha ahadi yake ya kuwaletea maji.

Naye Fatma Joseph, alisema ujenzi wa tangi hilo na vioski vitano vitawasaidia wananchi kupata huduma ya maji kwa uhakika.

Munge wa jimbo hilo, Mwambe alisema ujenzi wa tangi hilo ni moja ya utekelezaji wa ahadi zake alizokazitoa kipindi anaomba ridhaa ya kuwa mbunge na sasa ameitekeleza kama wajibu wake unavyomtaka kufanya.

Mwambe alisema ataendelea kuwa bega kwa bega na wananchi wa jimbo hilo ikiwa ni pamoja na kuwapatia huduma zote za msingi kama maji, afya, ujenzi wa miundombinu ya barabara na katika sekta ya elimu.

Naye Meneja wa Wakala wa Huduma za Maji Vijijini, (RUWASA) Wilaya ya Masasi, Juma Yahaya, alisema mamlaka hiyo itaendelea kuwahudumia wananchi wa vijijini ili kuhakikisha kila mmoja anapata huduma ya majisafi na salama.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, akishiriki kikao kazi pamoja maofisa ardhi wa Mkoa wa Iringa na Manispaa ya Iringa mwishoni mwa wiki kwa lengo la kuwakumbusha kutimiza wajibu katika utendaji kazi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliovamia mgodi wapewa saa 36 kuondoka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

ZAIDI ya watu 500 waliovamia mgodi wa dhahabu Tanzoz na kuchimba dhahabu katika Kijiji cha Imwelo, Wilaya ya Chato mkoani Geita wametimuliwa.

Akizungumza na watu waliovamia mgodi huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alisema anatoa saa 36 waondoke katika mgodi huo na atakayekaidi atakiona cha 'mtemakuni'.

Kwa upande wake Ofisa Madini mkoa huo, Laurent Bujashi, akizungumza na watu waliovamia mgodi huo alisema kutokana na hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Madini Dodoma, watu wote waliovamia wanatakiwa kuondoka kupisha mwekezaji huyo kuendelea na shughuli zake.

Meneja wa Kampuni ya mgodi huo, Amosi Mugendi, alisema anashukuru waliovamia wametii amri ya serikali ya kuondoka bila shuruti na kuacha mgodi ukiwa wazi.

Mugedi alisema mwekezaji huyo alishawalipa wananchi 126 na makaburi 68 fidia ya Sh. milioni 813 mwaka 2019 wote waliokuwa eneo la mgodi huo na baada ya fidia, alishangaa kuona watu kutoka maeneo mbalimbali zaidi ya 500 wakivamia mgodi huo na kuanza kuchimba dhahabu.

Alisema baada ya uvamizi huo Septemba, 2021 walienda kushtaki katika mahakama ya madini Dodoma na kesi ilisikilizwa na hukumu ilipotoka Kampuni ya Tanzoz ilipata ushindi.

Aidha, alisema baada ya mahakama hiyo kuwapa ushindi, bado watu hao waliovamia waliendelea na uchimbaji hadi Juni 30, mwaka huu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Mwaibambe alipofika na kutoa amri ya saa 36 kuondoka.

Nipashe ilishuhudia wamamizi hao wakikusanya vitu vyao na kuondoka bila shuruti.

# Singida kulima zaidi ya ekari laki 6 alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKOA wa Singida umepanga kulima ekari 627,391 za mashamba ya alizeti katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na tatizo la upungufu wa mafuta ya kula nchini.

Hayo yalielezwa juzi na Katibu Tawala msaidizi anayeshughulikia uzalishaji na uchumi Mkoa wa Singida, Stanislaus Chowaji, wakati wa kikao cha wakulima, wasindikaji, viongozi wa vyama vya ushirika, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na wataalamu wa kilimo kutoka wilaya zote za mkoa huo.

Kikao hicho kilikuwa mahsusi kwa ajili ya kujadili mstakabali wa kilimo cha alizeti Mkoa wa Singida ukiwa kati ya mikoa mitatu iliyowekewa mikakati na serikali kulima alizeti kwa wingi ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini. Mikoa mingine ni Dodoma na Simiyu.

Chowaji alisema ekari hizo zitalimwa na wakulima wadogo ekari 541,705, mashamba ya pamoja ekari 11,060, wakulima wakubwa ekari 14,885 na mashamba ya uwekezaji yatalima ekari 54,920.

Wengine ni vyama vikuu vya msingi vitalima ekari 420, Jeshi la Magereza litalima ekari 970, AMCOS ekari 2,591,mashamba ya vikundi ekari 550 huku shule za msingi na sekondari katika halmashauri zote za mkoa wa Singida zikitarajia kulima ekari 2,591 na hivyo kufanga jumla kuu ekari 627,591 zitakazolimwa msimu wa 2022/2023.

Alisema kutokana na ekari hizo 627,591 zitakazolimwa msimu huu wa 2022/2023, mkoa wa Singida utahitaji kupata mbegu tani 1254.5 ambalo ni ongezeko la tani 800.9 zilizotolewa na serikali tani 453.6 katika msimu wa 2021/2022.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Binilith Mahenge, alisema katika msimu wa 2021/2022 mkoa ulilima ekari 653,382.8 za alizeti na matarajio ya mavuno yalikuwa ni kupata tani 513.382, lakini kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango uzalishaji umeshuka na tani 272 zinatarajia kuvunwa.

"Bado kuna changamoto ya uhitaji wa mafuta ni mkubwa, hata mategemeo yetu tuliyokuwa tunategemea kuagiza nje mafuta bado huko nje nako hayajawatosha, hivyo tunatakiwa tuwe na namna ya kujikwamua katika hili kama mkoa," alisema.

Dk. Mahenge alisema Mkoa wa Singida vipo viwanda 243 vikubwa, vya kati na vikubwa vya kusindika mafuta, lakini malighafi haitoshi na ndiyo maana mwaka jana ukawekwa mkakati wa kuongeza uzalishaji kwani ardhi ya kutosha ipo.

Kwa upande wao wakulima wa alizeti waliiomba serikali kuwapatia mbegu bora za alizeti kwa kuwa waliyopewa msimu huu imewapa hasara kubwa kutokana na baadhi ya wilaya kutostawi na kushusha kiwango cha uzalishaji ikilinganishwa na misimu iliyopita.

"Wizara ya Kilimo ilipokuwa inatoa mbegu hizi kwa sisi wakulima kwani haikuona kuwa hazifai hadi imesababisha tumepata hasara kiasi hiki," alilalamika Milangton Musa mkulima kutoka Wilaya ya Mkalamo.

Naye Mkulima Hamis Said kutoka Wilaya ya Ikungi, alisema mpango wa serikali ulikuwa mzuri kuletewa mbegu ya ruzuku, lakini walicholetewa sio mbegu bali ni chakula.

"Hii tuliyoletewa ilikuwa sio mbegu kabisa, imetuongezea umaskini mkubwa wakulima nadhani hili lilifanyika kama kufunika kombe mwanaharamu apite," alisema.

Aidha, wakulima waliiomba serikali kabla ya kutoa mbegu ipime kwanza ardhi kila wilaya ili kujua udongo gani unafaa kwa kilimo cha alizeti na pia iongeze maofisa ughani kila kata.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Singida, alisema mkoa una kata 139 maofisa ughani waliopo ni 159 watakaogawanywa kila kata kuanzia sasa.

# RC awaonya wanaochelewa kazini

**Na Thobias Mwanakatwe,**

**IKUNGI**

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, amewaonya watumishi wa serikali mkoani hapo tabia ya kuchelewa kazini.

Amesema wafanyakazi hao wanaingia ofisini kwa kuchelewa, badala ya kuanza kufanyakazi, wanakimbilia kunywa chai na kuchezea simu huku wananchi wakisubiri kuhudumiwa.

Alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ikungi, ambao walimlalamikia kuwa katika Zahanati ya Ikungi kupatiwa matibabu mgonjwa anakaa zaidi ya saa sita bila kuhudumiwa huku wauguzi wakiendelea kupiga soga, kunywa chai na kuchati na simu.

"Watumishi kuchelewa kazini na kuanza kunywa chai wakati wa kazi sio sahihi, malalamiko kama haya yakiletwa kwangu tena na wananchi, wewe DMO (Mganga Mkuu wa Wilaya) nitakuweka pembeni," alisema.

Dk. Mahenge pia alionya tabia ya watumishi wa afya kuwaambia wananchi wanapokwenda kupata matibabu kwamba dawa zimeisha.

"Haya mambo yaliyosemwa na wananchi hapa sitaki kuyasikia tena, jana (juzi) mliniambia MSD (Bohari Kuu ya Dawa) wameleta dawa mkoa mzima kwa hiyo hamna sababu ya kuwaambia wananchi dawa hakuna," alisema.

Wakati huohuo, aliwatahadharisha wananchi kutouza chakula walichoweka akiba kutokana na maeneo mengi kutopata mvua za kutosha msimu huu.

Dk. Mahenge alisema kutokana na hali hii iliyopo ambayo inaonyesha dalili za upungufu wa chakula, wananchi wahakikishe wanalima mazao yanayoweza kustawi maeneo yenye unyevunyevu.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa kutokana na wananchi wengi katika wilaya yake kutovuna kutokana na ukosefu wa mvua, serikali ya wilaya imeanza kufanya tathmini ya kupata idadi ya wananchi ambao hawana chakula.




Mratibu Taasisi ya Mahusiano na Mawasiliano ya Umma nchini Tanzania (IPRT), Dk. Titus Simsamba (kulia), pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo cha Daystar, Prof. Laban Ayiro (kushoto), wakipongezana baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji (MOU) baina ya taasisi hizo ili kutoa mafunzo kuhusu mawasiliano ya kimkakati mahususi kwa watendaji wakuu, maofisa mawasiliano, maofisa utumishi pamoja na maofisa mbalimbali katika mashirika hapa nchini. Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IPRT, Daystar waingia ushirikiano kiutendaji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Mahusiano na Mawasiliano ya Umma Tanzania (IPRT), imesaini makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji na Chuo Kikuu cha Daystar, Kenya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya makubaliano hayo jijini Dar es Salaam, Mratibu wa IPRT, Dk. Titus Simsamba, alisema kupitia makubaliano hayo taasisi hizo zitashirikiana kutoa mafunzo kuhusu mawasiliano ya kimkakati kwa watendaji wakuu, maofisa mawasiliano, maofisa utumishi katika mashirika nchini Tanzania.

"Lengo kuu la makubaliano haya ni kuongeza ufanisi katika mafunzo tunayoyatoa kwa walengwa wa kozi zetu," alisema Dk. Simsamba.

alisema kupitia makubaliano hayo wadau wa mawasiliano na uongozi nchini wakiwamo waandishi wa habari watakuwa kwenye nafasi ya kushiriki mafunzo ya kujinoa kitaaluma yatakayotolewa na wataalamu kutoka Chuo cha Daystar.

"Habari njema ni kwamba hatua hii muhimu inakuja ikiwa ni siku chache tu tumetoka kukamilisha mafunzo ya kwanza kabisa kupitia programu hii tuliyoyafanya ndani ya wiki moja Morogoro, walengwa walipata wasaa kujifunza kozi mbalimbali ikiwamo mawasiliano ya kimkakati kwa taasisi na mashirika, mawasiliano wakati wa mgogoro," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo cha Daystar, Prof. Laban Ayiro, alisema makubaliano hayo ni mwendelezo wa mahusiano imara baina ya wananchi na serikali zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), hususani katika nyanja ya kitaaluma kupitia mawasiliano ya umma na uongozi.

Alisema ushirikiano huo mpya baina ya taasisi yake na IPRT utatekelezwa kwa urahisi zaidi kwa kuwa taasisi hizo zina nia ya pamoja ambayo ni kutoa mafunzo kwa wanataaluma wa mawasiliano ya umma na uongozi.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo yaliyofanyika Morogoro, Padri Masoke Edward, alisema yamekuja wakati muafaka kwa kuwa yamewajenga zaidi washiriki wakiwamo viongozi wa dini ambao wanakutana na kuwasiliana na makundi ya watu mbalimbali.

# CORECU yalaani utoroshaji ufuta

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MENEJA wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU), Mantawela Hamisi, amelaani kitendo cha baadhi ya watu kujihusisha na utoroshaji wa ufuta wakati minada ikiendelea katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mnada wa ufuta uliofanyika katika Kijiji cha Kingoma, Wilaya ya Mkuranga na kubainisha kuwa tani 1,500 za zai hilo ziliuzwa.

Alisema baadhi ya wadau wanatuhumiwa kufanya ulanguzi na utoroshaji ufuta kwa kuwarubuni wakulima, kununua kwa bei ndogo.

"Wananunua kutoka kwa wakulima kwa Sh. 1,200 kwa kilo moja wakati kwenye minada kilo moja inauzwa kwa zaidi ya Sh. 3,000, wakinunua ni vema wangekuwa wanauleta kwenye maghala ili tupate takwimu, lakini wao wanautorosha kwa njia za panya na kughushi nyaraka. Hii inaleta taswira mbaya kwa wanunuzi wengine," alisema.

Pia alisema jambo hilo hawatalifumbia macho, vyombo vya dola vitashughulika kwa yeyote atakayehusika kwa kuwa wanunuzi wa zao hilo wanapoongezeka inaleta tija kwa wakulima kuuza ufuta wao kwa bei nzuri.

Meneja wa ghala la kuhifadhia mazao lililoko Kijiji cha Kingoma, Jovin Bukori, aliwataka wakulima kuacha kurubuniwa na kuuza mazao yao kwa bei ya chini, kwamba mfumo wa ghala kwa sasa umekaa vizuri.

Aidha, aliwapongeza viongozi wa Wilaya ya Mkuranga kwa ushirikiano wa kufanikisha kukamata baadhi ya magari yaliyokuwa yanatorosha ufuta.

Meneja huyo pia aliwataka wakulima kuzingatia usafi kwenye ufuta wakati wakiujaza kwenye vifungashio sambamba na kuzingatia ujazo unaotakiwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika (AMCOS) cha Kiseese, Ayub Kamote, aliiomba serikali kuingilia kati kuweka mageti ya ukaguzi kwa ajili ya kudhibiti utoroshaji wa ufuta ambao unawaletea hasara wakulima.

Mmoja wa wanunuzi kutoka Kampuni ya SM Holding, Said Mkunga, alisema wakulima wa Mkoa wa Pwani wanatakiwa kuwa kitu kimoja kwa kufuata taratibu za uuzaji wa ufuta zinazotolewa na CORECU ili wapate faida.

## GEL kuwakutanisha wanafunzi 400 waliosoma nje

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI 400 waliosoma nje ya nchi wanatarajiwa kukutana jijini Dar es Salaam kwenye mahafali yao yaliyoandaliwa na Wakala wa Elimu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL).

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa GEL, Abdulamick Mollel, alisema kila mwaka wanafunzi wanaopata fursa ya kusoma nje ya nchi wanakaribishwa nyumbani ili wafurahie na wazazi wao, ndugu, jamaa, marafiki na watu waliokuwa wakiwalipia masomo.

Molel alitaja lengo lingine la kuwakutanisha kuwa ni kutengeneza daraja kwa kuwa wanafunzi wengi wanakuwa hawajulikani kwa watu wengine kama wawekezaji na waajiri na kwamba mahafali ni sehemu ya kunadi ujuzi na utaalamu ambao wameupata kwa waajiri.

"Wakati mwingine unaweza kukuta wawekezaji wana uhitaji wa aina fulani ya utaalamu, lakini wanakuwa hawawajui hivyo mahafali yanakuwa daraja la wale wenye kuhitaji vijana wanaotoka nje ya nchi kufanya nao kazi iwe mwekezaji kutoka nje au hata mwekezaji mzawa na tutakuwa na wahitimu takribani 200 wa fani ya udaktari," alisema Mollel.

Alisema mahafali hayo hutumika kutafuta fursa mbalimbali na ushahidi kwa wazazi Watanzania kwamba kuna vijana wanakwenda nje ya nchi kusoma na kurudi nchini kufanyakazi tofauti na fikra zilizokuwapo kwamba wakienda huko hawarudi.

"Mifumo na sera zetu baada ya kuwa imara vijana wetu sasa wanakwenda nje ya nchi kuchota ujuzi na maarifa na kurejea nchini kutumia ujuzi wao kuijenga nchi yao na wanakuja nchini kuangalia sehemu gani serikali na wawekezaji wanaweza kuwatumia kwa ujuzi walioupata," alisema Mollel.

Alisema wahitimu hao wangeweza kupata fursa ya kubaki kwenye nchi hizo kwasababu nchi nyingi zimewatengenezea mazingira ya kubaki huko kutokana na kutokuwa na rasilimali watu ya kutosha, lakini wanarudi kwa uzalendo wao kwa nchi.

Alisema baadhi ya vijana hao huja na watalii ambao ni marafiki zao na wawekezaji kutoka kwenye mataifa waliyotoka ambao wamevutiwa na taarifa za uwekezaji na mazingira mazuri ya biashara yaliyopo hapa nchini.

"Faida nyingine ya kuwafanyia mahafali ni networking, kwasababu unakuta kijana kasoma Malaysia, India, Canada, Mauritius, mwingine Marekani, Uingereza, Japan, lakini hawajuani hata kama walikuwa chuo kimoja sasa unapowakutanisha unatengeneza urafiki kwao. Kunakuwa na vijana ambao hawana fursa na wengine wanazo sasa wanakutana na kupeana mbinu," alisema Mollel.

Kwenye mahafali hayo huwaalika vijana wanaotarajia kwenda kusoma nje ya nchi na waliohitimu hutumika kama hamasa kwa wenzao.

Alisema kitendo cha kuwaona Watanzania wanahitimu vyuo vikuu nje ya nchi ni ushahidi kwamba elimu na maarifa yanayotoka nchini ni msingi bora na imara unaowawezsha vijana wanapokwenda nje ya nchi kufaulu kirahisi na kwamba GEL imekuwa ikiwaita wamiliki wa vyuo vikuu vya nje ambako vijana hao walisoma ili kushuhudia vijana wao wakifurahi na wazazi na jamaa zao.




Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, Alex Mgeni, akitoa maelezo ya namna ya kupata mkopo kupitia huduma ya Mshiko Fasta kwa wafanyabiashara wakubwa kwenye mtandao thabiti kwa ukuaji endelevu wa biashara, ili nao wakawaeleze wafanyakazi wao jinsi ya kukopa kupita simu zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi kushughulikia malalamiko usimamizi maliasili wazinduliwa

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, amezindua mfumo wa kushughulikia malalamiko (GRM) yatokanayo na utekelezaji wa shughuli za mradi wa kuboresha usimamizi wa maliasili na kukuza utalii Kusini (REGROW), iliyofanyika mkoani hapo ambao ni kitovu cha utalii kwa ukanda wa kusini mwa Tanzania.

Alisema mwishoni mwa wiki kuwa mfumo wa GRM utasaidia kushughulikia kwa ufanisi malalamiko kutoka kwa watu walioathiriwa au wenye uwezekano wa kuathiriwa na shughuli za mradi huo kama sehemu kuu ya kusimamia vihatarishi vya kiutendaji.

Dk. Chana alieleza katika kikao kuwa mfumo huo pia utawezesha watekelezaji wa mradi kushughulikia malalamiko kwa wakati na kwa uwazi ili kupata ushirikiano chanya kwa jamii.

Kikao hicho kilikuwa mahusus kwa ajili ya wadau kupata taarifa ya utekelezaji wa mradi wa REGROW na kuzindua mfumo wa kushughulikia malalamiko yatayojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi.

"Mfumo huu wa kushughulikia na malalamiko unaweza kufungua njia madhubuti za mawasiliano, kuonyesha kuwa mradi wa REGROW unajali kuhusu jamii na ustawi wake, kuzuia au kupunguza madhara makubwa yatokanayo na shughuli za mradi kwa jamii...," alisema.

Dk. Chana pia alisema malengo ya mfumo huo yatafikwa ikiwa malalamiko yatashughulikiwa vizuri na kuepuka kujirudia.

Watekelezaji wa mradi wanapaswa kutambua kuwa malalamiko ni mrejesho kutoka kwa umma/jamii/wadau kuhusu utekelezaji wa mradi. Ni muhimu kujifunza kutokana na mrejesho huo na kuchukua hatua madhubuti.

REGROW ni mradi wa serikali unaofadhiliwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa lengo la kuboresha usimamizi na uendelezaji wa vivutio vya utalii vilivyoko katika hifadhi za kipaumbele za Nyerere (Matambwe), Ruaha (RUNAPA), Mikumi, Udzungwa (UMNP) pamoja na Kilombero Nature Forest Reserve (KNFR).

Mradi huo pia umelenga kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, kuboresha maisha ya jamii inayozunguka hifadhi za kipaumble na kuboresha uhusiano kati ya jamii na hifadhi ili kufanikisha uhifadhi endelevu.

Mradi unatekelezwa na serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo Hifadhi za Taifa (TANAPA), Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) na Ofisi ya Maji Bodi ya Bonde la Maji Rufiji (RBWB).

Unalenga kupunguza umaskini nchini kwa kuongeza fursa kwa wananchi moja kwa moja kupitia utalii, kilimo cha kisasa na sekta nyingine ambazo zinazochangia uchumi wa nchi kama miundombinu na usafirishaji.

Dk. Chana alisema mradi huo unalenga kutoa ajira zaidi ya 40,000 kwa wakulima na wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi za kipaumbele na nyingine ambazo sio za moja kwa moja kwa Watanzania.

Mradi umepata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB) wa Dola za Marekani milioni 150 (zaidi ya Sh. bilioni 300).

Wabunge akiwamo wa Mafinga Mjini, Cosato Chumi, wamepongeza uzinduzi wa mfumo wa kushughulikia malalamiko mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za mradi wa REGROW ili kupata uhusiano chanya kwa jamii.

Walisema kuwa kutokana na ukubwa wa uwekezaji wa mradi huo, ni wazi kuwa shughuli za utekelezaji wa mradi zinagusa jamii, wanyama, mazingira, watumishi, watalii na wadau wengine ndani na nje ya eneo la utekelezaji wa mradi.

# Wafanyakazi wakumbushwa wajibu kuepuka misuguano

**Na Sabato Kasika**

KATIBU wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Mkoa wa Kinondoni jijini Dar es Salaam, Tushabe Bebwa, amewataka wafanyakazi kutimiza wajibu ili kuepuka misuguano kati yao na waajiri.

Alisema hayo mwisho mwa wiki katika hafla ya utoaji zawadi kwa wafanyakazi bora wa kiwanda cha kutengeneza mabomba ya chuma cha Tanzania Steel Pipe (TSP) kilichoko Ubungo.

Alisema ni muhimu kila mfanyakazi kuzingatia uhusiano bora sehemu ya kazi kwa kufuata miongozo, taratibu, kanuni na sheria za kazi ili iwe rahisi kudai haki.

"Hakutakuwa na shida kudai haki zenu iwapo kila mmoja wenu atakuwa ametimiza wajibu wake kikamilifu kwa kufuata miongozo ya kazi," alisema Bebwa.

"Uhusiano bora mahali pa kazi ndilo lengo la TUICO, huwezi kuwa unakwenda kinyume na taratibu au sheria kazi eti kwa sababu ni mwanachama wa chama hiki, mwajiri anabaki na haki yake ya kukuchukulia hatua," alisema.

Aidha, alisema zawadi walizokabidhiwa wafanyakazi bora, ziwe chachu kwa wote kufanya kazi kwa bidii, ili kuongeza uzalishaji, pia kujenga uhusiano bora na mwajiri.

"Kuna suala la mkataba wa hali bora, nyie kama wanachama, ni vyema mtajadiliana na mwajiri wenu, ila niwakumbushe wale ambao sio wanachama wa TUICO, hawawezi kuwamo katika suala la mkataba wa hali bora, hivyo niwaombe mjiunge na chama," alisema.

Ofisa Rasilimali Watu wa kiwanda hicho, William Msofe, alisema mwaka huu TSP imepata wafanyakazi wanane waliozawadiwa mabati 40 na vyeti.

"Kwenye suala la uchapakazi, sina tatizo na wafanyakazi wa kiwanda hiki, ila wapo wenye nidhamu mbovu, ambao nitashughulika nao ili kuwaweka kwenye mstari," alisema Msofe.

Alisema, suala la nidhamu ni muhimu mahali pote ikiwamo kazini, na uongozi hautavumilia wafanyakazi wenye utovu.

Mwenyekiti wa TUICO wa tawi la kiwanda hicho, Ernest Paul, aliwataka kuendeleza umoja kama njia mojawapo ya kumwezesha kuwa karibu na mwajiri ili wanapokuwa na jambo lao, iwe rahisi kusikilizwa na kitekelezewa.

"Umoja wetu ni jambo la muhimu, nami ninaahidi kuendeleza kutetea maslahi yenu, hivyo tuendelee kushikamana huku tukitimiza wajibu wetu kazini kadri inavyowezekana," alisema Paul.

## Wazanzibar watakiwa kudumisha tamaduni

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Mohammed Mazrui, amewataka Wazanzibar kuendelea kudumisha utamaduni wao ili vizazi vijavyo vijifunze.

Aliyasema hayo katika maonyesho ya 46 ya Biashara Kimataifa Dar es Salaam (DITF) ikiwa ni siku maalum ya utamaduni wa Zanzibar iliyoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE).

Alisema ni muhimu kwa Wazanzibar kutumia utamaduni wao ili kupunguza mmomonyoko wa maadili katika taifa.

Pia, alisema utamaduni una faida kubwa kwa sababu watalii wanatoka nje ya nchi kwa ajili ya kuangalia na kujifunza utamaduni wa Zanzibar.

"Hivi sasa Zanzibar tuna makabila mengi kama tukiendelea kuutangaza utamaduni wetu utatusaidia kuleta ushawishi kwa vijana wetu kutumia utamaduni wao," alisema Mazrui.

Kwa upande wake Ofisa Uhusiano Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hassan Haji Chumu, alisema kushiriki kwao katika maonyesho haya ya 46 kumezidisha wigo mpana wa kutangaza utalii wa ndani wa Zanzibar.

## TFS yatoa ofa maalum maonyesho DITF

WAKALA wa Huduma za Misitu (TFS), umetoa ofa maalum kwa wanaotembelea maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), kwenda kutembelea vivutio kwenye hifadhi za misitu asilia.

Akizungumza na Nipashe kwenye banda la TFS lililoko kwenye maonyesho hayo, Mkuu wa Kitengo cha Uhamasishaji Utalii wa Wakala huyo, Anna Lawuo, alisema wamefanya hivyo ili kutoa fursa kwa wanaotembelea maonyesho hayo kwenda kuona na kujifunza mambo mbalimbali yaliyoko katika vivutio hivyo ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utalii.

Alitaja baadhi ya vivutio ambavyo wametoa ofa kwa ajili ya kwenda kuvitembelea kuwa ni pamoja na Hifadhi ya misitu asilia ya Magamba, Amani, Pugu Kazimzumbwi, Vikindu, na Bagamoyo.

Alisema watalii watakaotembelea vivutio hivyo katika kipindi hiki cha ofa, watapelekwa kwa usafiri maalum, na gharama nyingine za kutembelea hifadhi ikiwamo chakula hawatatozwa pesa isipokuwa itatumika ofa ambayo watakuwa wamelipa.

"Kwa hiyo, hii ni fursa adimu hususani kwa watalii wa ndani, kuna vitu vingi vya kuona na kujifunza vilivyoko katika hifadhi zetu za misitu asilia, kwa hiyo ni vema wakachangamkia hili fursa," alisema Lawuo. "Pamoja na kwamba ofa hii ni kwa watalii wote, wa ndani na nje, lakini si vema wakawaachia wale wanaotoka nje ya nchi yetu pekee, kwa sababu unapokwenda kujifunza huko ni lazima utoke na mtazamo mpya na huwezi kuacha kwenda tena siku nyingine na inakusaidia hata kuwafundisha watoto na watu wengine mali asili zetu."

Alisema ofa hiyo ni kwa watalii watu wazima pamoja na watoto japokuwa gharama ni tofauti.

# 'Wanawake changamkieni fursa za serikali'

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Wanawake Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, amewashauri wanawake wajasiriamali kuchangamkia fursa zilizotengenezwa na serikali ya awamu ya sita.

Mwajuma alitoa kauli hiyo jana katika banda la TWCC kwenye maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimatafa ya Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imefungua fursa nyingi za kibiashara ambazo endapo wafanyabiashara watachangamka na kuzitumia ipasavyo watafanikiwa kuinuka zaidi kiuchumi.

"Fursa za biashara ambazo serikali ya Rais Samia imezifungua zimeleta matumaini makubwa hususani kwa wanawake wengi wafanyabiashara ambao walikuwa wamekata tamaa, walikuwa hawaoni mwanga, lakini kwa sasa naona kila mmoja anasema yuko tayari kufanya biashara," alisema Mwajuma.

"Kikubwa ambacho wanawake wanatakiwa kufanya ni kuchangamka, wafanye biashara kwa kuboresha bidhaa zaidi ili waingie kwenye soko la Kimataifa," alisema.

Pia Mwajuma alisema TWCC wamekuwa wakiendesha mafunzo mbalimbali kwa wanawake hao wajasiriamali namna ya kuendesha biashara zao na kuchangamkia fursa zinazojitokeza.

"Kwa mfano kabla ya kuanza maonyesho haya ya Sabasaba, tuliwapatia mafunzo kwanza ili kuhakikisha wanapokuja kushiriki wafahamu namna ya kuchangamkia fursa na hii ndiyo miongoni mwa siri zinazochangia sisi kufanya vizuri," alisema Mwajuma.

"Kwa hiyo wanawake kwenye banda letu wamekuja na bidhaa bora za hali ya juu, watu wanaopita humu kwenye mabanda wanashangaa sana kutokana na bidhaa hizo wanazozikuta humu, kwa kweli ni jambo la kushukuru."

Alitoa wito kwa wananchi kufika kwenye banda hilo la wanawake wajasiriamali kujionea na kujifunza kupitia bidhaa mbalimbali wanazozalisha.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Taifa, Dk. Nicolaus Shombe, akimsikiliza kwa umakini mhitimu na mjasiriamali kutoka Chuo cha Uhasibu (TIA) Isaya Maligite, alipotembelea Banda la Chuo hicho katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (TanTrade), jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MAHUMI**

# TIRA yaondoa kiwango akiba maalumu

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeondoa kiwango cha akiba maalumu ambacho kimekuwa kikitozwa kwa watoa huduma katika sekta hiyo.

Imesema imeamua kuondoa kiwango hicho kwa kuwa kimekuwa ni changamoto kubwa kwa watoa huduma hao.

Akizungumza na Nipashe, katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), Meneja wa TIRA, Frank Fred, alisema lengo la kuondoa kiwango hicho ni kutaka kuona sekta ya bima inakua zaidi na huduma inatolewa kwa watu wengi zaidi. Fred alisema awali gharama ya kujiunga kuwa wakala wa bima ilikuwa ni Sh. milioni 1.8, lakini wameiondoa baada ya kusikiliza ushauri wa serikali pamoja na wadau wa sekta hiyo.

"Tunafanya hivi kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kupunguza mrundikano wa tozo ili kutoa fursa kwa vijana wengi kufanya biashara," alisema Fred.

Alisema mpaka sasa wana kampuni ya uwakala zaidi ya 32 na endapo kila moja itatoa ajira 100 kwa vijana watakuwa wamepunguza tatizo hilo.

Kadhalika, alisema katika maonyesho hayo wanatoa elimu juu ya muongozo unaotoa fursa kwa kampuni za simu za mkononi kuingia ubia na wadau wa bima kwa kutumia simu za mkononi.

# 'Royal Tour' yatoa fursa Watanzania kwenda Iran

TANZANIA imejipanga kuchangamkia fursa za kibiashara zilizoko katika nchi ya Iran.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade), wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 40 ya ushirikiano wa Tanzania na Iran yaliyofanyika kwenye maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

Alisema bado kuna fursa nyingi za kibiashara zilizopo Iran ambazo Tanzania bado haijazichangamkia na kwa sasa wanajipanga kuzifikia.

Alisema tayari Ubalozi wa Iran umewaalika kwa ajili ya kwenda kufanya ziara nchini humo kuangalia fursa mbalimbali zilizoko. "Na huu mwaliko wa Iran umetokana na filamu ya Royal Tour iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo kwa sababu tulikuwa hatujachangamkia fursa kwenye nchi hiyo, tutapanga timu iende huko kwenda kuangalia fursa za kibiashara ambazo tutazitumia," alisema.

Kwa upande wake Kaimu Balozi wa Iran nchini, Hossein Bahineh, alisema wako tayari kuhakikisha uhusiano waliojenga kati ya nchi hizo unaendelezwa.

Alisema miongoni mwa fursa zilizopo Iran ambazo Tanzania inatakiwa kuzichangamkia ni pamoja na uwekezaji kwenye viwanda, gesi na madini.

Nipashe
Spotika



SEHEMU 8 AMBAZO NEYMAR ANAWEZA KWENDA KWA MKOPO UK. 12-13




LINGARD

# WACHEZAJI WATANO HURU MAN UNITED

**LONDON,** England

KLABU ya Manchester United imewaaga wachezaji 10 ambao mikataba yao ilimalizika saa 11:59 jioni ya Juni 30, mwaka huu.

Watano kati ya hao sasa ni wachezaji huru bila klabu, na watatu tayari wamesaini mikataba ya kujiunga na klabu nyingine na wengine wawili kustaafu kabisa soka.

Paul Pogba alikuwa jina kubwa zaidi kati yao, anaondoka bila malipo miaka sita baada ya United kumfanya Mfaransa huyo kuwa mchezaji ghali zaidi katika historia wakati huo kwa kumsajili kwa pauni milioni 89.

Pogba sasa anatazamiwa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Juventus kwa uhamisho wa bure, jambo la kushangaza kwa mara ya pili katika maisha yake ya soka, baada ya hapo awali kufanya uhamisho kama huo akiwa kijana mwaka 2012 wakati United ilipokataa kutimiza matakwa ya mkataba wake.

Jesse Lingard pia si mchezaji wa United tena, kwa mara ya kwanza alijiunga na akademi ya klabu akiwa na umri wa miaka saba na akaendelea kucheza michezo 232 ya kikosi cha kwanza kwa jumla baada ya mechi yake ya kwanza mwaka 2014.

Lingard alifika kilele msimu wa 2017/18 akiwa na mabao 13 katika michuano yote na alifunga bao la ushindi katika muda wa ziada kwenye fainali ya Kombe la FA mwaka 2016 katika uwanja wa Wembley.

Na alifurahia mkopo wa mafanikio kule West Ham. Mashabiki wa United wanaweza kukasirishwa zaidi na kuondoka kwa Juan Mata, ambaye alisalia kuwa mtu maarufu katika miaka yake nane na nusu hapo Old Trafford, licha ya kucheza mara chache na kidogo katika misimu ya hivi karibuni.

Mata alisajiliwa na United kwa pauni milioni 37.1 na alifunga mabao 10 katika mashindano yote katika kila msimu mitatu kamili ya kwanza katika klabu hiyo.

Edinson Cavani anaondoka United baada ya miaka miwili pekee. Mshambuliaji huyo mkongwe kwa muda mfupi alikuwa shujaa kutokana na mabao na uchezaji wake msimu wa 2020/21 - haswa katika kipindi cha pili cha msimu.

Cavani alikubali kuongezewa mwaka mmoja msimu uliopita wa joto, lakini kwa nia yake mwenyewe angeondoka kama angejua angeshindania nafasi kwenye timu na Cristiano Ronaldo.

Nemanja Matic alithibitisha kuondoka kwake United kwenye mtandao wa kijamii Mei. Ilifikiriwa kuwa Mserbia huyo bado alikuwa na mkataba wa mwaka mwingine, lakini baadaye ikaripotiwa kuwa klabu hiyo ilinukuu vibaya urefu wa mkataba huo wakati ulipotangazwa awali.

Matic tayari ameungana na Jose Mourinho kule AS Roma, klabu ya tatu tofauti ambayo wamefanya kazi pamoja baada ya United na Chelsea.

Mlinda mlango Lee Grant ameondoka katika klabu hiyo na kuamua kutundika daruga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, ambaye kimsingi alikuwa kipa chaguo la kwanza kwa timu ya Stoke, aliwasili Old Trafford mwaka 2018 kama chaguo la tatu.

Grant aliichezea United mechi mbili ndani ya miaka minne, ingawa mchango wake muhimu ulikuwa kwenye uwanja wa mazoezi. Hata alijifunza Kihispania ili kujenga uhusiano wenye nguvu na David de Gea na Sergio Romero.

Mchezaji mwingine ambaye amestaafu soka ya kulipwa ni Paul McShane. Beki huyo mkongwe alianza maisha yake ya soka Old Trafford na alikuwa mshindi wa Kombe la FA la vijana mwaka wa 2003, kabla ya kurejea katika majira ya joto mwaka jana kwa nia ya kujaza nafasi ya ukocha wa wachezaji waliozidi umri katika kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 23.

McShane haondoki United kabisa, amejiunga na wakufunzi katika timu za umri chini ya miaka 18 na 23. Safari ya United imekamilika kwa D'Mani Mellor, ambaye aliichezea klabu hiyo mara moja pekee katika kikosi cha kwanza, akiingia kwenye mchezo maarufu wa Ligi ya Europa dhidi ya Astana Novemba 2019 wakati kocha wa wakati huo, Ole Gunnar Solskjaer aliwaacha wengi wa kikosi cha kwanza.

Pamoja na wale nane ambao tayari wametajwa, wachezaji wengine wawili ambao hawakucheza katika kikosi cha kwanza pia wameiacha klabu kama wachezaji huru ni Reece Devine na Connor Stanley.

Wawili hao tayari wamesaini mikataba na Swindon na Bolton.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo ameripotiwa kuiomba klabu hiyo kumruhusu kuondoka ikiwa Mashetani hao Wekundu watapokea ofa sahihi wakati wa dirisha hili la usajili wa majira ya joto.



# SEHEMU NANE AMBAZO NEYMAR ANAWEZA KWENDA KWA MKOPO

**PARIS,** Ufaransa

KATIKA hali mbaya ambayo wachache sana wangetarajia wakati dirisha la usajili lilipofunguliwa, ni Neymar kuondoka Paris Saint-Germain msimu huu wa joto.

**Rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi amezungumza kwa uwazi kuhusu kutaka kuondoka katika enzi za wachezaji 'mabishoo' kwenye mji mkuu wa Ufaransa - ambapo bila shaka unahusishwa mshambuliaji huyo wa Brazil.**

Labda kwa kutabirika, maoni hayo yanasemekana kumkasirisha Neymar na kambi yake, na baadaye ikaripotiwa kwamba, anaweza kuondoka PSG.

Uhamisho wa kudumu unaweza kuwa mgumu kutokana na fedha ambazo zitahitajika ili kuondoka. Badala yake, wazo la mkopo limeelekezwa ambapo sehemu au mishahara yote ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ya euro milioni 35 itatolewa na klabu yake mpya.

Hapa tunaangalia sehemu ambazo Neymar anaweza kwenda kucheza kwa mkopo:

**BARCELONA**

Barcelona kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia mwelekeo wa Neymar kwa nia ya kumnasa arejee klabuni hapo, lakini kwa sababu moja au nyingine kurejea kwake hakujawahi kutimia licha ya kile ambacho kimekuwa kikionekana kutamaniwa mara kwa mara.

Sasa, kwa kuzingatia ugumu wa kifedha wa Blaugrana hao unaoendelea, hii inaonekana kama ndoto.

Barcelona wanajaribu kujiimarisha licha ya kuwa na bajeti ndogo. Hata hivyo, kuna uwezekano mdogo wa Neymar kutua hapo.

**BAYERN MUNICH**

Klabu ya Bayern Munich ni moja ya timu nyingine ambayo imekuwa ikihusishwa mara kwa mara na Neymar kwa miaka kadhaa.

Bayern wamemsajili mchezaji bora wa dunia Sadio Mane na nyota huyo wa zamani wa Liverpool na anacheza eneo sawa na la Mbrazil huyo. Sio kama hawajajaa vizuri katika idara hiyo pia, huku wakiwa na wakali kama Serge Gnabry, Kingsley Coman na Leroy Sane, bado wanaweza kumhitaji Neymar.

Uwezekano wa kuondoka kwa Robert Lewandowski kwenda Barcelona kunaweza kutengeneza nafasi ya kutua kwa Neymar.

**CHELSEA**

Kwa sasa kuna majina machache sana ambayo hayapo kwenye rada za mmiliki mpya wa Chelsea, Todd Boehly, na anaweza kuona fursa ya kumpata Neymar kuwa nzuri.

Chelsea imekuwa klabu inayotajwa mara kwa mara kwamba inaweza kuingiza nia ya kumtaka mshambuliaji huyo - jambo ambalo mchezaji mwenzake wa kimataifa Brazil, Thiago Silva anatamani zaidi litokee.

Hata hivyo, kocha wa zamani wa PSG, Thomas Tuchel haaminiki kuwa na nia ya kumchukua Neymar hapo Stamford Bridge, badala yake anawalenga Raphinha, Raheem Sterling na Ousmane Dembele.

**NEWCASTLE**

Ikiwa kuna klabu moja ambayo ina fedha na (pengine) ina nia ya kupata wachezaji wakubwa basi ni Newcastle United.

Kwa kuwa tayari wametumia fedha nyingi Januari, wamiliki wapya watakuwa wakitafuta saini ya nyota wakubwa.

Jina la Neymar halilingani sawa na Kieran Trippier, Bruno Guimaraes na Nick Pope. Iwapo wanataka kufanya mporomoko mkubwa ili kupuliza kila kitu kingine kutoka kwenye maji bado haijaonekana.

**MANCHESTER CITY**

Klabu nyingine ambayo jina lake mara nyingi limekuwa likihusishwa na klabu hiyo imeibuka tena katika wiki za hivi karibuni.

Mchezaji huyo hajawahi kuficha nia yake ya kufanya kazi pamoja na bosi maarufu wa City, Pep Guardiola.

Ingawa hii ndiyo aina ya usajili ambayo uongozi wa Man City ungetamani katika miaka ya awali ya uongozi wao, pengine wamevuka hitaji la uhamisho.

Mafanikio ya hivi karibuni ya Man City yamejengwa juu ya misingi ya timu inayofanya kazi kwa bidii, na yenye mshikamano, badala ya kutegemea nyota mmoja.

Kuwasili kwa Erling Haaland kunaweza kubadili hilo na kuondoka kwa Gabriel Jesus kunatengeneza nafasi kwenye kikosi, lakini katika hatua hii kuongezwa kwa Neymar hakutahisi kama hatua ya kusonga mbele.

**MANCHESTER UNITED**

Ikiwa kuna klabu moja ambayo inapenda uhamisho wa fedha nyingi ni Manchester United - lakini kwa mara nyingine tena fursa hii labda imekuja kwa kuchelewa sana.

Kocha mpya Erik ten Hag bila shaka atakuwa akitafuta kuondoka kutoka kwa aina za usajili ambazo zimeelemea United tangu kuondoka kwa Sir Alex Ferguson na kuchangia kumaliza kwao vibaya Ligi Kuu msimu uliopita.

Kwa kuzingatia matatizo yao ya nje ya uwanja na misururu na mastaa wanaolalamika, kuleta ubinafsi mkubwa katika soka la dunia kwenye bodi haionekani kuwa jambo la busara.

**MLS**

Ingawa kuhamia 'nyumba ya kustaafu ya mpira' kunaweza kuonekana kuwa mapema zaidi kwa Neymar, hivi karibuni alifichua kuwa 'angependa' kucheza Ligi Kuu ya Marekani, MLS mara tu atakapoondoka PSG.

Huenda likawa swali tu iwapo anahisi kuwa hana biashara ambayo haijakamilika Ulaya kwa wakati huu, huku Mbrazil huyo akijulikana kuwa na hamu ya kushinda tena Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**REAL MADRID**

Real Madrid kwa muda mrefu imekuwa na ndoto ya kumsajili Neymar - hata alipokuwa mchezaji wa Barcelona. Lakini pamoja na klabu nyingine kwenye orodha hii, hamu hiyo imepungua katika miaka ya hivi karibuni.

Mchezaji mwenzake wa PSG, Kylian Mbappe sasa ni mboni ya jicho la Los Blancos na bila shaka watamtafuta Mfaransa huyo tena msimu wa joto wa 2023.

Mshindi wa mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Vinicius Jr, anaonekana kuwa lulu zaidi pale Bernabeu na anaonekana kuwa na uhakika wa kufikia au kuzidi ushujaa wa maisha ya Neymar.

Real inaonekana kuwa na nafasi kwenye mkono wa kulia, lakini tayari imependekezwa kuwa Neymar sio chaguo ambalo wanafikiria.



NEYMAR

## Nukuu

"TUMEZUNGUMZA na Paul Pogba, mambo yanaendelea vizuri sana na uwepo wake hapa Juventus pia utakuwa wa msingi kutoka kwa mtazamo wa kibiashara." **Mkurugenzi Mtendaji wa Juventus, Maurizio Arrivabene**



"INTER Milan imenipa mengi na ninatumaini kufanya vyema zaidi wakati huu. Sasa ni wakati wa kufanya kazi kwa bidii kama kikosi na tunatumaini kuwa bora zaidi kuliko hapo awali." **Romelu Lukaku**



"TUNATAMANI sana kumbakisha. Ninatumaini kwamba, atachagua Bayern Munich. Ikiwa mchezaji hataki kuamua kwa klabu, basi tunaweza kutafuta suluhu ambayo itamfurahisha kila mtu." **Mkurugenzi wa Bayern, Hassan Salihamidzic kuhusu Serge Gnabry**





# REKODI ZA KUKUMBUKWA LIGI KUU 2021/22

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 ilimalizika Jumatano iliyopita, ikishuhudia Yanga ikitwaa ubingwa bila kupoteza mechi yoyote.

**Ilimaliza ligi ikiwa na pointi 74 baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Kwenye ligi hiyo imeshuhudia timu za Mbeya Kwanza ikiwa ya kwanza kushuka daraja na kwenye mechi ya mwisho, Biashara United iliungana nayo baada ya kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Straika wa Geita Gold, George Mpole akatwaa kiatu cha dhahabu kwa kuwa mfungaji bora msimu 2021/22, akipachika mabao 17, akimzidi bao moja straika wa Yanga, Mkongomani Fiston Mayele aliyemaliza akiwa na mabao 16.

Timu za Mtibwa Sugar na Prisons zimekwenda kucheza mechi ya mchujo, 'play off',

Timu hizo sasa zitalazimika kucheza mechi mbili za 'play off' nyumbani na ugenini. Jana zilitarajiwa kucheza mechi ya kwanza ya mchujo.

Baada ya mechi ya marudiano, timu iliyoibuka mshindi wa jumla itabaki Ligi Kuu, na itakayofungwa itakwenda kucheza mechi nyingine ya mchujo na timu kutoka Ligi ya Championship ambayo tayari imeshapatikana, JKT Tanzania.

Yoyote itakayocheza na JKT Tanzania mechi za nyumbani na ugenini, ikishinda itabaki Ligi Kuu, lakini ikifungwa itashuka daraja na kwenda Championship na kuwapisha JKT Tanzania ambao wakishinda wanapanda.

### MABAO 471 YAFUNGWA

Jumla ya mabao 471 yamefungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu 2021/22, kati ya hayo 35 yakiwa yamepatikana kwa mikwaju ya penalti.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, jumla ya penalti 67 msimu huu zimepatikana, 35 zikitiwa kambani, 14 zikiota mbawa na 18 zikiokolewa au kudakwa na makipa.

Kati ya mabao hayo 23 ni ya wachezaji kujifunga wenyewe.

### SIMBA KINARA KUKOSA PENALTI

Timu ya Simba imekuwa kinara wa kukosa mikwaju ya penalti kwenye Ligi Kuu iliyomalizika. Imekosa penalti tano, ikifuatiwa na Geita Gold na Biashara United ambazo zimekosa penalti mbili kila moja.

Pia kwenye ligi hiyo, jumla ya kadi nyekundu 24 zimetolewa kwa wachezaji mbalimbali kutokana na utovu wa nidhamu.

### MNATA AONGOZA KUOKOA PENALTI

Kipa wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata, Hamadi Kadedi wa Mbeya Kwanza na Khomein Abubakar wa Geita Gold wote wameweka rekodi ya kuokoa penalti mbili kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Makipa waliookoa penalti moja moja ni Aboutwalid Mshery wa Yanga, A Salula wa Azam, na James Ssetuba wa Biashara United, na Mohamed Makaka wa Ruvu Shooting.

### HAT-TRICK TATU TU

Ni wachezaji watatu waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja, 'hat-trick' kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Straika wa Prisons, Jeremiah Juma ndiye aliyekuwa wa kwanza kufunga 'hat-trick', Novemba 27, mwaka jana kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Sumbawanga, alipofunga mabao yote matatu, na kuipatia timu yake ushindi wa mabao 3-1.

Wakati mashabiki wengi wakidhani msimu huu kungeweza kuwa na 'hat-trick' moja tu, siku chache kabla msimu kumalizika, Shiza Kichuya wa Namungo alipiga ya kwake Juni 26 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, akiibeba timu yake kupata ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya wenyeji Matibwa Sugar.

Siku ambayo pazia la Ligi Kuu linafungwa Jumatano iliyopita, straika Mkongomani, Idriss Mbombo naye alifunga 'hat-trick' yake, ikiwa ni ya tatu na ya mwisho msimu huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, akiiwezesha timu yake ya Azam FC kushinda mabao 4-1 dhidi ya Biashara United.

### DIARRA AONGOZA KWA 'CLEAN SHEETS'

Kipa wa Yanga aliyesajiliwa msimu huu, Djigui Diarra raia wa Mali ameongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, akifanya hivyo mara 15, akifuatiwa na kipa mwenzake wa timu hiyo, Abutwalib Mshery, ambaye amepata 'clean sheets' 12, lakini zingine akitoka nazo kwenye timu yake ya zamani, Mtibwa Sugar.

Kipa wa Simba Aishi Manula ameshika nafasi ya tatu kufanya hivyo mara 11 msimu huu.

### LUSAJO, MUSSA WAZEE WA 'ASSIST'

Straika wa Namungo, Reliants Lusajo, ambaye ilidhaniwa kuwa huenda akatwaa kiatu cha dhahabu baada ya kuanza kwa kasi mwanzoni mwa Ligi Kuu, lakini akakomea kwenye mabao 10, yeye amekuwa kinara wa kutoa pasi za mwisho zilizozaa mabao 'assist', akifanya hivyo mara sita, sawa na Abdurahman Mussa wa Ruvu Shooting aliyewahi kuwa kinara wa mabao msimu wa 2016/17, akiwa pamoja na Simon Msuva wakati huo akiichezea Yanga, wote wakifunga mabao 14.

Mussa na Lusajo wamewapiku Fiston Mayele na Djuma Shaaban wa Yanga, Pape Sakho wa Simba, na Pius Buswita wa Ruvu Shooting.

### JE, WAJUA?



BAADA ya kusaini mkataba wa miaka mitatu wa kuendelea kuwatumikia Liverpool hadi mwaka 2025, Mohamed Salah sasa atakuwa analipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki. Mshahara huo unaokadiriwa kuwa sawa na shilingi milioni 982 kwa wiki utamfanya Mmisri huyo kuwa mchezaji wa Liverpool anayelipwa ghali zaidi.





## Klabu za wanafunzi wapinga rushwa kuimarishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa usimamizi wa maadili kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Leila Mavika, ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mikoani kuanzisha na kuziimarisha klabu za wanafunzi za wapinga rushwa shuleni ili kujenga jamii inayochukia vitendo hivyo.

Mavika alitoa rai hiyo jana kwenye fainali ya mashindano la mdahalo kuhusu mapambano dhidi ya rushwa kwa wanachama wa klabu za wapinga rushwa za shule 28 za sekondari za Jiji la Dodoma.

"Kwenye utumishi wa umma kitachohitajika ni utaalamu, uaminifu na uwajibikaji na ninaamini kuwa endapo tutaimarisha klabu za wapinga rushwa utaweza kupata watumishi wa umma wa baadaye watakaokuwa na hivi vigezo," alisema.

Alibainisha kuwa ni lazima kila mwananchi awe mzalendo kwa nchi yake kwa kupinga vitendo vya rushwa, anaamini kama itaimarisha nguvu hiyo kuanzia ututoni watafanikiwa kujenga kizazi chenye maadili.

Aliipongeza TAKUKURU Mkoa wa Dodoma kwa kuja na ubunifu wa mashindano hayo ambayo atawaimarisha wanafunzi kuvichukia vitendo vya rushwa na kupata viongozi waadilifu wa baadaye.

Awali, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema mashindano hayo yalianza mwezi Aprili, mwaka huu na yakishirikisha shule za sekondari 28 kati ya 54 zilizoko jijini humo.

Kibwengo alisema mada katika mdahalo huo ilikuwa ni udhibiti wa vitendo vya rushwa katika miradi ya maendeleo na ililenga kuwajengea uwezo wananchi na jamii katika kusimamia miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa katika maeneo yao.

Alisema fedha zinazotumika katika miradi ya maendeleo ni kodi za wananchi na kupitia mashindano hayo wanawajengea uwezo wanafunzi kutambua na kuwa na uelewa katika kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye miradi.

"Tunaamini kuwajengea uwezo watoto hawa watakwenda kutoa elimu katika maeneo yao na watakwenda kuelimisha jamii zinazowazunguka kupata uelewa wa kudhibiti vitendo vya rushwa katika miradi na usimamizi wa miradi hiyo," alisema.

Alisema mashindano hayo yalilenga kuwajenga vijana mapambano dhidi ya rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa na watumishi wa umma wa baadaye wenye maadili kwenye utumishi wao.

Kibwengo aliwasisitiza shule zilizopata ushindi kuendelea kuwa mabalozi wazuri katika klabu za kupinga rushwa ili kuhakikisha inatokomezwa.

"Tunaomba mwendelee kuwa mabalozi wazuri wa masuala ya rushwa, mmeanza mkiwa shule tunaomba mwendelee kuwa mabalozi hadi maeneo mnayoishi," alisema Kibwengo.



Wakazi wa Mtaa wa Mwaja Kata ya Chamwino katika Jiji la Dodoma wakifanya usafi kwenye mtaro ulioko kandokando ya barabara ya Wajenzi hadi Nkuhungu juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Serikali kusimika mitambo 57 hewa Oksjeni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inatarajia kusimika mitambo 57 ya kuzalisha hewa tiba ya Oksjeni kwenye Hospitali za Rufani za Mikoa, Kanda na wilaya nchini,

Aidha, ameitaka Hospitali ya Benjamin Mkapa ambayo inazalisha hewa hiyo kuuza kwa bei nafuu ili kuokoa maisha ya watu.

Ummy aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua mtambo wa kisasa wa kuzalisha hewa hiyo uliosimikwa katika hospitali hiyo.

Alisema usimikaji wa mitambo hiyo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya awamu ya sita katika kuhakikisha kuwa huduma zinaboreshwa na kuongeza kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita mitambo 14 imesimikwa kwenye hospitali za rufani za mikoa nchini.

"Sisi kama sekta tumejiwekea vipaumbele vyetu ambavyo Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ingependa kuviona tunavitekeleza, kipaumbele kikubwa ni ubora wa huduma za afya, hivyo mitambo hii ina lengo la kuokoa maisha kwa wananchi wake," alisema.

Alipongeza hospitali hiyo pamoja na Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Alphonce Chandika kwa kuhakikisha kuwa kazi ya usimikaji wa mtambo huo unakamilika kwa wakati na unazingatia viwango vinavyotakiwa.

"Huu mtambo hautasaidia hospitali hii tu bali hata hospitali na vituo vya mikoa wa Dodoma na mikoa ya jirani ikiwamo Manyara, Singida na Iringa," alisema.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. bilioni 1.5 ambao unazalisha mitungi 400 ya Oksjeni kwa siku.

"Hapo kabla ya UVIKO-19 hospitali ilikuwa inatumia mitungi 200 kwa mwezi, lakini ilipokuja UVIKO-19 mitungi 200 inatumika kwa siku," alisema.

"Nawaomba pia muanzishe mpango wa matengenezo wa mtambo huu, nisingependa kusikia mnazalisha baada ya muda mchache mtambo unakufa."

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema mtambo huo una sehemu mbili ambazo hazitegemeani inayoweza kuwasha sehemu moja kipindi inatumia ili kuhakikisha uzalishaji unaendelea wakati wote hata wakati wa matengenezo kinga inapolazimu kuzima upande mmoja.

Dk. Chandika alisema kipindi cha UVIKO-19, matumizi ya hewa hiyo yaliongeza gharama za uendeshaji wa hospitali na ilikuwa ikitumika Sh. milioni 10 kwa siku badala ya kwa mwezi.

"Sh. bilioni 1.5 zimetumika kununua mitambo miwili aina ya Ozcan Kardesler Tip Cihazlari San, mitungi ipatayo 560 ya hewa tiba, gari la kusambazia mitungi ya Oksjeni pamoja na ujenzi wa jengo ambalo mitambo imefungwa," alisema.

## Halmashauri kukaguliwa utoaji zabuni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema itaanza kukagua utoaji zabuni kwenye halmashauri ambazo hazitoi kwa kampuni za vijana na badala yake zinatoa kwa wanaowapa asilimia 10.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo katika hafla ya ugawaji wa vifaa mtaji kwa vikundi vya vijana na watu wenye ulemavu waliowezeshwa mafunzo kupitia programu ya taifa ya ukuzaji ujuzi.

Alisema agizo la Rais Samia Suluhu Hassan na Sheria ya Manunuzi inataka asilimia 30 ya zabuni kwenye halmashauri zipewe kampuni za vijana.

"Tutapita mikoani kukagua na kwa kuwa TAMISEMI mpo hapa na ndiyo mabosi wa chini kule tusaidiane kuhakikisha kampuni za vijana zinapewa tenda, yale masuala ya kuangalia wale ambao wanatoa ten percent yamekuwa yakitokea."

"Sasa kuanzia leo nasema kabisa tunaenda kusimamia vijana kampuni zao zipewe tenda kwenye halmashauri na mabaraza ya madiwani yasimamie hili na sisi tutapita kuangalia, tunataka kampuni za vijana zipewe tenda," alisema.

Katambi alisema kama kampuni zitakuwa hazijapata usajili na zina upungufu zisaidiwe ili wawe na sifa ya kupewa zabuni hizo.

"Tunafahamu wale wanaotoa tenda kwenye halmashauri mnachukua hadi zile asilimia ambazo vijana wanapaswa kupewa, tukisimamia hili vijana wengi wa kitanzania watanufaika," alisema.

Kuhusu vifaa hivyo, alisema ofisi hiyo imeamua kuanzisha utaratibu wa kugawa vifaa mtaji na kwa mwaka huu zimenunuliwa cherehani 400, seti 75 za mashine za uchomeleaji na uungaji vyuma pamoja na seti 70 za mashine za kutengeneza vifaa vya aluminiamu.

"Vifaa hivi vimegharimu Sh. milioni 371 na vitagaiwa kwa vijana hao ili kuvitumia kuzalisha zaidi, lakini ni mkakati wao wa kujiajiri, ofisi yetu imekuwa ikitekeleza programu mbalimbali za vijana kwa kushirikiana na wadau mbalimbali," alisema.

Alisema ofisi hiyo ilishirikiana na TAMISEMI kuweka vigezo vya kuwapata vijana watakaopewa vifaa hivyo ikiwamo wenye ulemavu, kujiunga kikundi na vikundi vinavyorejesha mikopo kwa wakati kwenye halmashauri zao.

Awali, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema vifaa hivyo vimetolewa vya fani ya ushonaji nguo, uchomeleaji na utengenezaji wa vifaa vya aluminum.

Alisema vimetolewa kwa vijana 1,741 waliopo kwenye vikundi zaidi ya 175 kwenye mikoa 26.

Hata hivyo, alisema vijana walikuwa wakiwezeshwa mitaji ya fedha na wengine walikuwa wakitumia kwa malengo yasiyokusudiwa.

Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Serikali za Mitaa kutoka TAMISEMI, Humphrey Mniachi, alisema ugawaji wa vifaa unatekeleza dhana ya ugatuaji madaraka.



# Wakulima kahawa wapewa mafunzo udhibiti wadudu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATAALAMU wa kahawa wameanza kuwafikia wakulima wa zao hilo, kuwapa elimu ya kupima afya ya udongo lengo ni kupambana na wadudu waharibifu na kuongeza uzalishaji.

Msimamizi Mkuu wa Shamba la Kahawa Utengule Coffe, Amani Ngowi, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu namna walivyojipanga kuwafikia wakulima ili kupambana na ongezeko la kemikali kwenye udongo.

Ngowi alisema kwenye utafiti wao wamebaini wakulima walio wengi kushindwa kuzalisha kahawa kwa wingi kutokana na kutopima afya ya udongo, kutokujua aina ya mbolea inayohitajika na kufanya kilimo cha mazoea na wengine kutojua jinsi ya kuzuia magonjwa ya kahawa shambani.

"Kuna magonjwa mengi yanatokea kwenye kahawa lakini wakulima wengi hawafahamu mfano mwaka jana ugonjwa wa hawa wadudu wadogo walitokea lakini wakulima hawakufahamu jinsi ya kukabiliana nao, tunashauri wakulima wapate elimu juu ya kilimo cha kisasa pia serikali iwasaidie wakulima wapate mbegu bora za kahawa," alisema Ngowi.

Mmoja wa wakulima wa kahawa, kutoka Utengule -Usongwe Upendo Sailosi, alisema kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la wadudu kwenye mimea ambao wanatoboa miti na kuifanya isistawi bali kuoza.

Alisema kuwa Siku ya Mkulima ni msaada kwao kwa sababu wanakutana na wataalamu na maofisa ugani kupata elimu ya namna kukabiliana na wadudu na magonjwa mengine pamoja na kuzalisha kwa tija.

Mkulima mwingine, Peter Mwashitete alisema mafunzo hayo yatawasaidia namna ya kuotesha mbegu kisasa, kukata miti ya kahawa pamoja na uchumaji hadi hatua ya kuvundika.

Alisema Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), imewasaidia kupata mafunzo na usimamiaji mzuri wa zao hilo, kwa kuhakikisha ubora na minada inasimamia bei elekezi iliyoko sokoni.

Meneja wa Kanda ya Mbeya wa TCB, Sijali Boa, alisema katika kuwafikia lengo la kuwasaidia wakulima wameamua kuanzisha siku ya mkulima ili kuwasogezea karibu wakulima, maofisa ugani na wadau wengine wanaohusika kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Alisema matarajio yao baada ya mafunzo hayo ni kuona wakulima wanazalisha kwa kuzingatia kanuni za kilimo na kujikwamua kimaisha kupitia kilimo hicho.

# Wakazi Ziwa Nyasa watakiwa kulinda vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WATANZANIA wanaoishi kanda ya mito inaoingia katika Ziwa Nyasa, wametakiwa kuongeza bidii katika utunzaji wa vyanzo vya maji ya mito hiyo.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi Elice Engelbert, wakati akizungumza kwenye kikao cha bonde hilo kilichofanyika jana Tukuyu Mjini wilayani Rungwe.

Mhandisi Engelbert alisema wakazi hao ndiyo wameshika uhai wa Kamisheni ya Mto Zambezi, inayoundwa na nchi nane.

Alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa asilimia 59 ya maji yote kutoka Ziwa Nyasa yanazalishwa upande wa Tanzania, asilimia 33 ya maji hayo yanazalishwa Malawi, huku Msumbiji ikizalisha asilimia nane tu ya maji yote ya ziwa hilo.

Mhandisi Enfelbert alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nane zinazounda Kamisheni ya Mto Zambezi na kutokana na mchango huo wa maji katika Ziwa Nyasa, inakuwa ni nchi muhimu kwa uhai wa kamisheni hiyo.

"Nchi yetu inaumuhimu mkubwa katika Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi kutokana na mchango wetu katika uzalishaji wa maji ya Ziwa Nyasa, mchango huu unatokana na sisi Watanzania kutunza vyanzo vya maji, hivyo tunapaswa kuongeza bidii ili vyanzo hivyo viendelee kuwa salama kwa uhai wa kamisheni yetu ya Mto Zambezi," alisema Mhandisi Engelbert.

Baadhi ya wadau wa Bonde la Ziwa Nyasa, walisema tayari wameshaanza kuchukua hatua kuhakikisha kuwa wanahifadhi vyanzo vya maji kwa kuhakikisha shughuli zote za kinadamu zinazofanyika kwenye vyanzo hivyo zinasitishwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema anawatumia wataalamu wake kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa ikiwamo kuhamasisha upandaji wa miti rafiki kwenye vyanzo vya maji. "Tumeshaanza kuwaondoa watu wote waliojenga kwenye vyanzo vya maji, lakini pia tunawahamasisha wananchi wetu kupanda miti rafiki kwenye vyanzo vya maji ili kuvilinda," alisema Mchau. Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alitoa maelekezo kwa wataalamu wa halmashauri pamoja kuhakikisha wanalinda vyanzo vya maji kwa kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema katika baadhi ya maeneo wameweka alama kuzunguka vyanzo vya mito mbalimbali ambako eneo kubwa la ardhi inayotumiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo inaonekana iko ndani ya vyanzo hivyo.

Alisema katika maeneo hayo serikali haina mpango wa kuwaondoa wananchi, isipokuwa wanawahamisha kupanda mazao ya kudumu kama vile parachichi ili kutunza maeneo hayo na kulinda vyanzo vya maji.



Mlengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini wa Kata ya Kitwiru, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Ndalingwa Mwindichuma, akieleza namna TASAF ilivyomwezesha kuboresha maisha yake wakati wa ziara ya kikazi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama iliyolenga kukagua utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini katika halmashauri hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aruhusu mabasi kufanya safari usiku, mchana

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameruhusu mabasi ya abiria kufanya kazi saa 24 ili kuwawezesha wafanyabiashara kusafiri na kufanya shughuli zao nyakati zote , ili kukuza uchumi wa Jiji hilo.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye Kongamano la Nishati na Madini lililowahusisha wachimbaji wa madini, wakuu wa wilaya, wakurugenzi, wakuu wa idara na wataalamu wa madini.

Alisema kwa sasa ameruhusu mabasi yaanze kufanya safari kutoka jijini Mbeya kwenda mikoa mingine hususani Dar es Saalam ili kukuza uchumi na kuongeza mzunguko wa fedha.

"Baadhi ya maeneo kuna majadiliano kwamba ni marufuku magari madogo pamoja na magari aina ya costa kufanya safari saa 24, sasa ili kukuza uchumi wa Jiji letu, tumeagiza mabasi makubwa ndiyo yaanze kufanya safari saa zote, wafanyabiashara wa madini wa bidhaa mbalimbali ruksa sasa," alisema Homera.

Aidha, aliwahamasisha pia wamiliki wa hoteli na baa kufanya shughuli zao saa 24 ili kusaidia watu kupata huduma za chakula na vinywaji nyakati zote kuliko ilivyo sasa baadhi ya maeneo wanawahi kufunga.

Alisema kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wanaandaa utaratibu kuwabana wamiliki na madereva wa mabasi kupunguza mwendo nyakati za usiku ili kuepukana na ajali na maafa mengine yanayoweza kuhatarisha usalama wa abiria.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema Jiji la Mbeya linazidi kukua na kwamba ili uchumi wa wananchi wake uimarike lazima biashara zifanyike mchana na usiku.

Alisema wanaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa utulivu na kuongeza pato la Jiji hilo ambalo limebarikiwa kuwa na fursa mbalimbali za kukuza uchumi.

Baadhi ya wafanyabiashara wa madini akiwamo, Emmanuel Mbasha alisema wamefarijika serikali kuruhusu mabasi kufanya safari zake usiku na kwamba itasaidia kusafirisha bidhaa hizo nyakati zote. Aliiomba serikali kuimarisha ulinzi na usalama kwenye barabara korofi ili kuhakikisha usalama wa abiria na mali zao kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.





Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akibadilishana hati na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (E-Government ), Said Seif Said, muda mfupi baada ya kutiliana saini ya makubaliano ya ushirikiano wa Huduma ya Malipo kwa Mtandao baina ya Benki ya CRDB na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (E-Government), utakaolenga kuboresha huduma zitolewazo kwa wateja na Watanzania kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kurahisisha ukusanyaji mapato, malipo ya taasisi za serikali na binafsi ikiwamo ada na kusaidia ukuaji wa utalii kwa kuwa na kituo kimoja cha makusanyo (one centre collection). Hafla hiyo ilifanyika jana kwenye Hoteli ya Park Hyatt, Unguja, Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi CCM watakiwa kuwa mfano ulipaji mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) visiwani hapo umetakiwa kuwa mfano katika kuhamasisha ulipaji wa mapato kwa wafanyabiashara ili kuongeza uelewa kwa wananchi katika suala hilo.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, katika ufunguzi wa jengo la maduka ya biashara ofisi kuu ya CCM, Kisiwandui.

Alisema kuwa kukamilika kwa maduka hayo kutatoa fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kuwa na eneo la kisasa la kufanyia biashara zao ambalo litasaidia kuongeza mapato kupitia wafanyabiashara hao. Dk. Mwinyi alieleza kuwa ni jambo la kupongezwa kwa Chama Cha Mapinduzi kujenga maduka hayo hatua ambayo itasaidia kuongeza kipato kwa chama na kupunguza ruzuku pamoja na michango ya wahisani ili kuendesha vyema shughuli mbalimbali za chama. Aidha, alisema katika mradi huo kutatoa ajira zitakazosaidia kufikia azma ya serikali kuzalisha ajira zaidi ya 300,000 ndani ya muda wa miaka mitano. Vile vile, alisema juhudi za wafanyabiashara na taasisi binafsi zinasaidia serikali kuwapatia ajira Wazanzibari ili kujipatia kipato cha kila siku.

Mjumbe huyo wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, alikemea tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wanaokodishwa maduka na baadaye kukodisha wengine kwa bei ya juu na kueleza kuwa wafanyabiashara aina hiyo wachukuliwe hatua stahiki ikiwamo kufutiwa mikataba na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Naye Kaimu Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Kombo Hassan Juma, alisema kuwa ujenzi wa maduka hayo ni kusimamia azma ya CCM kuongeza vyanzo vya uchumi ndani ya chama hicho na kupunguza utegemezi.

Alisema CCM Zanzibar imejipanga kujenga maduka mengine ya ghorofa ili kuendana na kasi ya majengo mazuri na yenye kukidhi vigezo.

Akisoma taarifa ya ujenzi huo, Katibu wa Kamati Maalum Uchumi na Fedha ya CCM, Afadhali Taibu Afadhali, alisema ujenzi wa maduka 47 na huduma zingine ni kuunga mkono utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2020-2025 na kukamilika kwake kutatoa ajira zaidi ya 100.

# Waliokuwa wakijisaidia baharini sasa watumia vyoo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, amesema matumizi ya vyoo katika mkoa huo yameongezeka na kufikia asilimia 75, awali hali haikuwa ya kuridhisha kutokana na wananchi kujasaidia baharini na msituni.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu mafanikio, maendeleo na changamoto katika mkoa wake kwa muda wa miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi.

Alisema Wilaya ya Micheweni ambayo ipo katika mkoa wake ilikuwa ikiongoza kwa matumizi madogo ya choo kwa Zanzibar na Tanzania Bara ni Wilaya ya Katavi, lakini kwa sasa wananchi wa Micheweni wamehamasika na wanatumia vyoo.

"Kwa sasa huwezi kumuona mtu anaenda kujisaidia habarini matumizi ya vyoo yameongezeka kutokana na elimu tunayoitoa kuhusu matumizi ya choo na kuwa na choo kunaletea heshima," alisema.

Aliwapongeza wataalamu wa Wizara ya Afya kwa kutoa elimu ya umuhimu wa vyoo na kuhamasisha jamii matumizi nafuu na sahihi ya vyoo yanasaidia kuepukana na maradhi mbalimbali ikiwamo ya mlipuko.

Aidha, alisema hivi sasa mkoa wake umejenga matundu ya 661 kwa shule 51 na hali hiyo imepunguza tatizo la utoro kwa wanafunzi shuleni.

"Kukosekana kwa vyoo shuleni kulichangia utoro mkubwa kwa wanafunzi kwa sababu mtoto anatoka shule anaenda kujisaidia msituni au pwani na huwa harudii tena shule, lakini kwa sasa changamoto hii tumeitatua kwa kiasi fulani," alisema.

Alikiri kuwa utoro wa wanafunzi upo kwa baadhi ya maeneo hasa Wilaya ya Micheweni, lakini serikali inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuwarejesha shule watoto hao kupitia mradi maalum wa kuwarejesha shule.

Akizungumzia kuhusu vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto, alisikitishwa na vitendo hivyo ambapo changamoto kubwa iliyopo katika Mkoa wake watuhumiwa wa makosa hayo hukimbia baada ya kugundulika kufanya unyama huo.

"Mkoa wangu umepakana na nchi jirani ya Kenya hasa kwa Wilaya ya Micheweni, changamoto tunayoipata watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji hukimbia kisiwani Pemba na hukimbilia kusikojulikana," alisema.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuacha muhali katika kutoa ushahidi wa matukio hayo na kuwafichua wahalifu wa vitendo hivyo ili wafikishwe katika vyombo vya sheria na haki itendeke.

Alisema kesi 177 za udhalilishaji zilizoripotiwa katika vituo vya polisi katika mkoa wake zikiwamo za ubakaji 86, saba zimepata hatia, 31 zipo mahakamani, sita zimeondolewa mahakamani, 34 zimefutwa na polisi na 56 zinaendelea na upelelezi.

# TAMWA yahamasisha jamii uwezo kutambua haki

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amesema jamii iliyo na uwezo wa kutambua upungufu na kubaini changamoto zinazokwamisha upatikanaji wa haki zao ndiyo msingi wa ufikiwaji fursa sawa za kimaendeleo kwa njia ya kidemokrasia katika jamii.

Alisema kuwa jamii inakabiliwa na matatizo mbalimbali yanayokwaza haki na maendeleo yao, lakini zinashindwa kuyatatua kutokana na kukosa uwezo thabiti wa kuyazungumzia katika ngazi husika ili kufanyiwa kazi kwa wakati.

Dk. Mzuri alisema hayo wakati akizungumza na wahamasishaji jamii kudai haki zao na wanawake kushiriki katika masuala ya uongozi na demokrasia, kisiwani Pemba kupitia mradi wa kushajihisha wanawake katika uongozi.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano ya TAMWA, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na Jumuiya ya Utetezi wa Mazingira na Jinsia Pemba (PEGAO) kwa ufadhili wa Ubalozi wa Norway nchini.

Alisema, iwapo jamii itakuwa na uwezo wa kuyaibua matatizo yanayowakabili na kuchukua hatua sahihi itasaidia kuchochea uwajibikaji katika upatikanaji wa haki zao.

Alihimiza wahamasishaji jamii hao ambao wanafanya kazi katika wilaya zote nne za Pemba, kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kuwasaidia wananchi kuwa na uwezo wa kuibua matatizo yanayowakabili na kuyatafutia ufumbuzi kwenye vyombo husika.

"Dhana ya mradi kuunda wahamasishaji jamii ni kuhakikisha yule mwananchi wa chini awe na uwezo wa kuyaibua matatizo yanayomkabili, kisha kuchukua hatua dhidi ya matatizo hayo na kuwa na ujasiri wa kukaa meza moja na mamlaka husika kutafuta ufumbuzi kwa njia ya demokrasia," alisema Mzuri.

Aidha, alisema uwapo wa wahamasishaji hao katika jamii unalenga kuwafanya watoa huduma wa taasisi mbalimbali kuongeza kasi ya uwajibikaji dhidi ya utatuzi wa vikwazo vinavyowakabili wananchi kwenye maeneo yao.

Akiwasilisha ripoti ya uhamasishaji jamii kudai haki zao, Ali Othman, ambaye ni mhamasishaji jamii Wilaya ya Micheweni, alisema kupitia mikutano iliyofanyika kwenye shehia mbalimbali walibaini kuwapo baadhi ya changamoto ikiwamo uelewa mdogo wa wanawake katika masuala yatakayowasaidia kuingia kwenye nafasi za uongozi jambo ambalo linakwamisha ushiriki wao kikamilifu katika nafasi hizo.

Aidha, alibainisha changamoto nyingine ni uwapo wa vyeti feki vya kuzaliwa kwa baadhi ya wananchi wa Shehia ya Shumba, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba, jambo ambalo linasababisha wananchi wengi kukosa haki zao za msingi ikiwamo nafasi za uongozi.

"Tatizo la uwapo wa vyeti feki vya kuzaliwa kwa wakazi wa Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba ni moja ya changamoto kubwa tuliyoibua kwenye jamii, kwani katika mikutano yetu kwenye shehia wananchi wengi hasa Shehia ya Shumba Mjini kilio chao ilikuwa ni kupata vyeti feki," alieleza mhamasishaji huyo.

Alisema uwapo wa wahamasishaji hao katika jamii umesaidia kujenga uwezo kwa jamii kuwa na uthubutu wa kuzungumza matatizo yanayowakabili kwa uwazi.

Naye Husna Khamis, kutoka Wilaya ya Wete alieleza, baada ya kubaini kuwapo kwa tatizo la kutojua kusoma na kuandika kwa wananchi wengi hasa wanawake, walishirikiana na jamii kuanzisha madarasa ya watu wazima ili kuwapatia fursa wananchi kuondokana na tatizo hilo linalowakosesha haki zao muhimu.

Kwa upande wake, ofisa tathmini na ufuatiliaji kutoka ZAFELA, Rajab Hamad, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na wahamasishaji hao kwa kufanikisha ufuatiliaji wa changamoto na vikwazo vinavyochelew-

# Benki NBC yawapiga jeki wakulima mikopo trekta

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imezindua rasmi huduma ya utoaji wa mkopo wa trekta kwa wakulima katika Mkoa wa Ruvuma na mikoa ya jirani kwa lengo la kuwawezesha kuboresha shughuli za kilimo katika ukanda huo.

Mkopo huo ambao ni sehemu ya huduma ya NBC shambani, unaotolewa kwa masharti nafuu na mteja atalipa asilimia 25 ya mkopo kama malipo ya awali na kiasi kilichobaki atalipa kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mitano kulingana na makubaliano.

Akikabidhi moja ya trekta kwa mteja wa kwanza kupata huduma hiyo, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Ruvuma, Bakari Ally Mketo, aliipongeza NBC kwa kuanzisha huduma hiyo ambayo alisema itawawezesha wakulima kupata matrekta kwa urahisi zaidi na kusaidia katika kuongeza uzalishaji mkoani humo.

Alisema Mkoa wa Ruvuma ni moja kati ya mikoa inayochangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini na huduma hiyo itawawezesha wakulima kuboresha kilimo na kufanya sekta hiyo kuongeza tija zaidi nchini.

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, mkoa huo una jumla ya hekta 4,007,746 za ardhi zinazofaa kwa kilimo na katika kipindi cha miaka mitano 2015/2020, mkoa umezalisha tani 8,547,816 za mazao hadi kufikia mwaka 2020.

Meneja wa tawi la NBC Songea, Frank Kiranga, alisema huduma hiyo ni mahsusi kwa wakulima wa aina zote Mkoa wa Ruvuma na mikoa jirani na imelenga kuwawezesha kuongeza ufanisi wa shughuli za kilimo mkoani humo.

"Ili kupata huduma hii, mteja atatakiwa kuwa na shamba kuanzia hekari moja ambalo lina hati ya kimila au hati ya Kamishna wa Ardhi au mkataba wa mauziano na pia mteja atatakiwa kulipa malipo ya awali ya asilimia 25 na kiasi kilichobaki atalipa kwa awamu kuanzia mwaka mmoja hadi miaka mitano," alisema.

Chacha Mwikwabe, wa kwanza kupata huduma hiyo aliishukuru NBC kwa kuanzisha huduma hiyo na kumwezesha kutimiza ndoto ya kumiliki trekta ambayo itamwongezea kasi ya uzalishaji katika shughuli zake.

Trekta moja lina thamani ya Sh. milioni 62 na asilimia 25 ni sawa na Sh. milioni 15.5 ambayo ni malipo ya awali.




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, akipimwa afya kwenye banda la Vodacom AfyaCall na waganga, Kelvin Katamboi (kulia) na Peter Ngaiza wa kitengo cha AfyaCall juzi kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara Kimataifa (Sabasaba). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Pwani awapa kibano watendaji Rufiji

**Na Julieth Mkireri,**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameagiza watendaji wa Wilaya ya Rufiji walioruhusu mifugo kuingia katika wilaya hiyo bila kufuata utaratibu wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wafugaji Ikwiriri, Wilaya ya Rufiji na kueleza kuwa kukiukwa kwa taratibu za kupokea mifugo katika wilaya hiyo kumechangia migogoro ya ardhi.

"Mkuu wa wilaya mwelekeze mkurugenzi achukue hatua za kinidhamu kwa mtendaji aliyehusika kukiuka taratibu na kanuni za kuingiza mifugo Rufiji na kuanzia sasa mifugo isiruhusiwe kuingia tena," aliagiza Kunenge.

Pia aliwaonya wakulima kuwaingiza wafugaji kwenye maeneo yao na kwa yeyote anayehitaji majani wakishavuna wakate na kuwapelekea na sio kuwaruhusu kuingiza mifugo kwenye mashamba yao.

Aliwataka wakulima na wafugaji kufuata taratibu kwa kuepuka kuvunja sheria na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na serikali katika kumaliza migogoro kwenye maeneo yao.

Akizungumzia suala la mifugo kuvalishwa hereni, Kunenge alisema utaratibu huo utawezesha kuitambua na kudhibiti wizi.

"Mimi ndiyo niliomba hereni zianzie Mkoa wa Pwani na wafugaji kwenye maeneo waliyotengewa kila mmoja apate kitalu chake. Ninataka ufugaji bora uanzie Pwani wengine waje wajifunzie hapa," alisema.

Kunenge alisema mifugo iliyopo katika Mkoa wa Pwani inatakiwa kuhesabiwa ijulikane idadi na utaratibu wa hereni utarahisisha kila mmoja kuipata ikipotea.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, alisema wilaya hiyo ina mifugo zaidi ya 100,000, huku eneo la wafugaji likiwa ni hekta 56.

Meja Gowele alisema kwa sasa wanaendesha operesheni ya kuhakikisha mifugo inakaa katika maeneo iliyotengewa kuepusha migogoro.

Mmoja wa wafugaji, Martine Kindesheni aliwataka wafugaji kufuata maelekezo ya Serikali, huku baadhi ya wafugaji kuiomba serikali kuwapunguzia gharama ya kununua hereni kwenye kila mfugo kutoka Sh. 1,750 hadi Sh. 500.

# Mgeja apongeza viongozi dini kuliombea taifa

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Taasisi ya Tanzania Mzalendo Foundation, Khamis Mgeja, amempongeza Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Church of God International (T.C.G.I), Saimon Nkwabi na madhehebu mengine nchini kwa kazi ya kuendelea kuliombea taifa.

Askofu Mkuu wa kanisa hilo lenye makao makuu yake Kata ya Nyihogo, Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, alimtembelea mwenyekiti huyo jana ili kubadilishana mawazo na kufanya mazungumzo ya mustakabali wa nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Taasisi ya Tanzania Mzalendo Foundation inajishughulisha na masuala ya haki, demokrasia na utawala bora.

Mgeja ambaye ni mwanasiasa mkongwe, ameonyesha nia ya kugombea nafasi ya kiti cha mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga.

"Mimi nakupongeza wewe askofu kwa niaba ya makanisa yanayotoa huduma za kiroho katika wilaya yetu na Manispaa ya Kahama kwa kunikumbuka, lakini kubwa hasa kuombea viongozi wetu wa kitaifa ili wafanye shughuli zao za kuliletea taifa maendeleo," alisema.

Askofu huyo pia aliwaombea viongozi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Makamu wake, na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ili kuendeleza na kudumisha amani ya nchi na hatimaye kujiletea maendeleo kwa haraka.

"Sisi viongozi wa dini tutaendelea kuliombea taifa hili usiku na mchana, pia kumwombea Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kuendelea kuliongoza taifa letu kwa amani, upendo na usawa," alisema Askofu Nkwabi.

Aliwaomba Watanzania, wanasiasa na makundi mbalimbali kuendelea kumuunga mkono kwa kazi nzuri anayoifanya ya maridhiano kama taifa pamoja na kuleta maendeleo kwa nyanja mbalimbali.

Alifanya maombi mafupi ya kumtakia heri Mgeja katika maisha yake na kumwomba Mungu amzidishie hekima na busara, amkinge na shari yoyote.

"Nikupongeze tu mwenyekiti kwa kuwa mpenda haki na mkweli na unayependa kushirikiana vyema na jamii yote bila ubaguzi wa dini ukabila na ukanda watu wengi naomba waige mfano wako," alisema askofu huyo.

Maombi hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Manispaa ya Kahama na Halmashauri ya Msalala na Ushetu, wakiwamo na baadhi ya wazee akiwamo Katibu Mkuu wa Chama cha Kutetea Haki za Wanaume nchini, Antony Sollo.

## Mikakati mitatu NATO kukabiliana na Russia dhidi ya Ukraine

**MADRID,** Hispania

JUMUIYA ya Kujihami ya Nchi za Magharibi (NATO) imetangaza mpango wake mpya katika kukabiliana na uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine, ndani ya mfumo wa mkutano wa kilele uliofanyika Juni 29 na 30 mwaka huu, Madrid, Hispania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC mradi huo unajumuisha uwepo mkubwa wa wanajeshi wa Marekani barani Ulaya, hasa mashariki mwa bara hilo, pamoja na kifurushi cha usaidizi cha kina kwa Ukraine, ambacho kinajumuisha mafuta, vifaa vya matibabu, fulana zisizo na risasi na mifumo ya kuzuia ndege zisizo na rubani.

Shirika hilo la kijeshi pia lilitoa taarifa juu ya mkakati wake, nyaraka ambayo inaweka mkakati wake wa kijeshi na usalama kwa miaka 10 ijayo, ikielezea kwa undani vitisho vinavyokabili demokrasia ya Magharibi na kuelezea jinsi nchi za Magharibi zinakusudia kukabiliana navyo.

Shirika la Mkataba wa Atlantiki ya Kaskazini (NATO) ni muungano wa kijeshi wa kujihami ulioanzishwa mwaka 1949 na nchi 12, zikiwamo Marekani, Canada, Ufaransa na Uingereza, ambapo wanachama wake walikubali kuja kusaidiana katika tukio la shambulio la silaha dhidi ya nchi yoyote mwanachama.

Moscow pia inaiona NATO kama tishio na iliishutumu Jumatano kwa kuwa na kile walichokiita matamanio ya kifalme na kujaribu kusisitiza ukuu wake kupitia mzozo wa Russia na Ukraine.

Wakati huo huo, Rais wa Marekani, Joe Biden alisisitiza kwamba NATO inahitajika zaidi sasa kuliko hapo awali. **BBC**

**Moscow pia inaiona NATO kama tishio na iliishutumu Jumatano kwa kuwa na kile walichokiita matamanio ya kifalme na kujaribu kusisitiza ukuu wake kupitia mzozo wa Russia na Ukraine.**

# Wahamiaji haramu 53 wafariki dunia kwa joto

**TEXAS,** USA

NYARAKA za Mahakama ya Shirikisho nchini Marekani zinasema wahamiaji 53 waliokuwa ndani ya lori wakisafirishwa jijini Texas wamefariki kutokana na joto huku mshukiwa na dereva wa gari husika akidai kuwa hakujua kwamba kiyoyozi kiliacha kufanya kazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na BBC, hilo ni tukio baya zaidi la usafirishaji haramu wa binadamu katika historia ya Marekani.

Taarifa zilisema katika gari hilo pia kulikuwa na watoto kadhaa waliopatikana ambao wanaendelea kutibiwa hospitalini, huku ikielezwa kuwa waathiriwa walikuwa wanatoka Mexico, Honduras, El Salvador na Guatemala.

Pia kulingana na hati za mahakama ya shirikisho, mtoa habari wa siri wa serikali anayefanya kazi katika Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha na polisi wa Texas aliwaambia maofisa kwamba Zamorano na Martínez ambao ni miongoni mwa washukiwa walikuwa wamezungumza baada ya vifo hivyo kuripotiwa.

Inadaiwa Martínez alinukuliwa akisema kuwa "Dereva hakujua kitengo cha viyoyozi kiliacha kufanya kazi na ndiyo sababu watu hao walikufa," alisema.

Nyaraka zinaongeza kuwa mdokezi na Martínez walikuwa wamesimama ndani ya mita kadhaa kutoka kwa kila mmoja wakati mazungumzo hayo yalipofanyika.

**Usafirishaji wa watu ni tasnia kuu kwenye mpaka wa Marekani na Mexico. Pia Mei mwaka huu, rekodi ya wahamiaji 239,000 wasio na hati walizuiliwa wakivuka kuingia nchini humo wakitoka Mexico.**

Vile vile washukiwa wote wawili wanakabiliwa na hukumu ya kifo iwapo watapatikana na hatia ya makosa ya magendo na kula njama.

Aidha, nyaraka hizo zinaeleza kuwa wanaume wengine wawili wanaotuhumiwa kuhusika, Juan Claudio na Francisco D'Luna-Bilbao, wamefunguliwa mashtaka ya kumiliki silaha na kuwa nchini Marekani kinyume cha sheria ambao wote wawili ni raia wa Mexico.

Watu wengine walioathiriwa katika tukio hilo ni pamoja na raia 27 wa Mexico, pamoja na 14 kutoka Honduras, saba kutoka Guatemala na Wasalvador wawili.

Mamlaka ya Mexico ilisema jumla ya wahamiaji 67 walikuwa ndani ya lori, wakati waendesha mashtaka huko San Antonio wameweka idadi hiyo kuwa ni 64.

Alieleza kuwa ofisi ya mchunguzi wa afya ya Kaunti ya Bexar, ilisema imewatambua waathiriwa sita kati ya 53 kutokana na tukio hilo, akidai kuwa vitambulisho vinavyowezekana 42 vimefanywa huku watano wakiwa bado hawajatambulika.


Pia alisema Ijumaa ya wiki iliyopita, ofisi ya Sherifu wa Kaunti ya Bexar ilianza kuchunguza lori ambalo lilionekana kutelekezwa lililopatikana katika eneo la makazi maili chache na ambapo gari la kwanza lilipatikana.

Usafirishaji wa watu ni tasnia kuu kwenye mpaka wa Marekani na Mexico. Pia Mei mwaka huu, rekodi ya wahamiaji 239,000 wasio na hati walizuiliwa wakivuka kuingia nchini humo wakitoka Mexico.

Pia vifo vingi vya aina hiyo vimefichuliwa mara kadhaa ulimwenguni katika siku za hivi karibuni. Miongoni mwa kesi mbaya zaidi ni Austria, Agosti 27, 2015 ambapo lori lililotelekezwa lililosajiliwa na Hungary lilipatikana likiwa na miili 71 ya wahamiaji wa Iraq, Syria na Afghanistan.

Miaka mitatu baadaye, wanaume wanne walipokea vifungo vya miaka 25 jela nchini Hungaria kuhusiana na vifo hivyo, pia Libya Februari 20, 2017 makumi ya wahamiaji wa kiafrika walipatikana wakiwa wamefungiwa kwenye kontena la meli, wakiwamo watu 13 ambao walikuwa wamekosa hewa hadi kufa.

Nyingine ilitokea Uingereza Oktoba 23, 2019 ambapo jumla ya wahamiaji 39 wa Kivietnam walipatikana wamekufa kwenye trela la lori huko Essex. Na wanaume wanne walifungwa jela kwa kuua bila kukusudia Januari 2021. **BBC**



Mwonekano wa lori lililokuwa limebeba wahamiaji waliofariki dunia kutokana na joto huko Texas. **PICHA: BBC**

# Papa Francis asikitishwa safari yake kuahirishwa

**VATICAN,** Italy

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki, Papa Francis ameonyesha kusikitishwa na kitendo cha safari yake ya kuzuru Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Sudan Kusini, kuahirishwa kwa sababu za kiafya.

Kwa mujibu wa ujumbe wa video alioutoa jana, kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 85 alisema, anasikitika kuwa hataanza ziara hiyo katika mataifa hayo mwezi huu kama ilivyokuwa imepangwa, lakini akaongeza kuwa hivi karibuni atafanya ziara hiyo.

Papa Francis amesema anaifikiria Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwa sababu ya mateso ya wananchi wake, hasa katika eneo la Mashariki kwa sababu ya kukosa usalama, huku akitoa wito wa amani nchini Sudan Kusini ambayo pia imeendelea kushuhudia mauaji ya raia.

Mwezi uliopita, Vatican ilitangaza kuahirisha ziara ya kiongozi huyo wa Kanisa Katoliki, kwa sababu za kiafya kwa ushauri wa madaktari wake ambao walisema ziara hiyo ingetatiza matibabu yake.

Mbali na Afrika, ziara yake nchini Lebanon iliahirishwa lakini mpango wake wa kwenda nchini Canada mwishoni mwa mwezi huu, umeratibiwa. **RFI**

# AKPAN: NIMESHAAGA RASMI COASTAL UNION

Na Saada Akida, ARUSHA

KIUNGO wa kati wa Coastal Union, Victor Akpan amewaaga rasmi mashabiki wa timu hiyo na amesema mchezo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) dhidi ya Yanga ulikuwa wa mwisho kucheza ndani ya kikosi cha timu ya Tanga.

**Akpan ambaye amehusishwa kusajiliwa na Simba kwa mkataba wa miaka miwili kutumikia klabu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Nyota huyo alitumia fainali hiyo ikiwa ni mechi yake ya mwisho kuwaaga mashabiki wa Coastal katika mchezo huo na Yanga kushinda kwa mikwaju ya penalti ya 4-1 baada ya kukamilika dakika 120, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Akizungumza na gazeti hili jana, Akpan alisema mechi hiyo imekuwa rasmi kwa ajili ya kuwaaga mashabiki wa Coastal kwa sababu msimu ujao hatakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo.

Alisema malengo yake makubwa ni kutoka Coastal kwenda sehemu nyingine kwa ajili ya kutafuta changamoto nyingine na suala la muda itajulikana ni wapi atacheza hapa Tanzania au nje ya nchi.

"Wapi naenda ni suala la muda tu, kuhusu kuhusishwa na Simba mashabiki zangu wanatakiwa kuwa na subira kwa sababu ni muda mfupi tu kila kitu kitakuwa wazi ni wapi naenda."

"Kuhusu Simba kama nilivyosema awali ni timu kubwa sana kwa hapa Afrika Mashariki na kati, msimu huu hawakufanya vizuri lakini wako katika rekodi nzuri katika mashindano ya kimataifa," alisema Akpan.

Kiungo huyo alisema ana uhakika na uwezo wake uwanjani hali ambayo anaweza kucheza timu yeyote hapa hata nje ya Tanzania hali ambayo sasa ameamua kutoka Coastal na kwenda kutafuta changamoto zingine.

Alisema kuhusu kupoteza fainali dhidi ya Yanga alisema imewaumiza wachezaji wote kwa sababu walipambana hadi dakika za mwisho na hatimaye kutolewa katika hatua ya penalti.



Wasanii wa Bendi ya Mwalimu wakitumbuiza katika uzinduzi wa kampuni ya kutunza mazingira ya PETCO jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga, Simba kukutana Agosti 13*



Na Saada Akida, Arusha

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu ujao itaanza Agosti 17, na kumalizika Mei 27, sasa hatimaye Yanga na Simba zitakutana kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii itakayopigwa Agosti 13, 2022 Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Miamba hiyo ya Kariakoo itakutana katika ufunguzi wa ligi hiyo baada ya matokeo ya fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) ambapo bingwa wa ligi ambaye ni Yanga amelibeba taji hilo.

Kwa mujibu wa kanuni za Bodi ya Ligi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) mchezo wa Ngao ya Jamii utapigwa kati ya Yanga dhidi ya Simba iliyomaliza nafasi ya pili katika Ligi Kuu.

Kanuni ya kucheza mechi ya Ngao ya Jamii inaeleza, bingwa wa FA atacheza na bingwa wa Ligi Kuu Bara ambao ni Yanga, lakini kama bingwa wa ligi ndiye huyo huyo bingwa wa FA, mshindi wa pili wa ligi atakipiga na bingwa wa ligi.

Akizungumza na gazeti hili, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo alisema ligi itaanza wakati usajili wa wachezaji ukiendelea ambao ulifunguliwa Julai Mosi na kufungwa Agosti 30 mwaka huu.



## Kaze: Fainali ya FA ilikuwa ya kibabe

Na Saada Akida, ARUSHA

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze (pichani), amesema fainali ya Kombe la FA ilikuwa ngumu na amewapongeza wachezaji kupambana katika mchezo dhidi ya Coastal Union.

Alisema katika michezo ambayo wamecheza katika mashindano ya msimu huu, fainali hiyo dhidi ya Coastal ilikuwa ngumu na ushindani mkubwa kwa ufundi na mbinu za makocha.



"Ilikuwa mechi ngumu sana, Coastal Union walicheza vizuri, wachezaji walipambana, na tulikosa nafasi nyingi, kikubwa hatukukata tamaa," alisema Kaze.

"Hii ni fainali tulitakiwa kupambana na tuliongeza watu wengine ambao walibadilisha mchezo na kuweza kusawazisha, penalti haina mwenyewe pia natakiwa kumpongeza sana golikipa Djoid Diara amepambana sana."

Alisema kuhusu Dennis Nkane ni mchezaji mzuri aliingia na kubadilisha mchezo na alifanya kazi kubwa hasa kulingana na umri wake, lakini amefanikiwa kupambana na presha za mashabiki.

"Kabla ya kumpa nafasi katika mchezo wa jana (juzi) tuliongea naye na tukamwambia anatakiwa kujiamini katika mechi hii na akifanya kile alichoambiwa na tukafanikiwa kupata ubingwa," aliongeza Kaze.

## Mkandala apewa miaka miwili Azam

Na Shufaa Lyimo

UONGOZI wa Klabu ya Azam FC, umetangaza kumpa mkataba wa miaka miwili mchezaji Cleofance Mkandala ambaye alikuwa anaichezea timu ya Dodoma Jiji.

Akizungumzia usajili huo ofisa habari wa klabu hiyo, Thabit Zakaria alisema wamesajiliwa nyota huyo ili kuipa nguvu timu hiyo, baada ya kutokufanya vizuri msimu uliopita.

"Mkandala anakuja kuitumikia Azam akiwa kama mchezaji huru tunaamini ataleta ushindani kwenye kikosi chetu msimu ujao," alisema Zakaria.

Alisema mchezaji huyo ataungana na wachezaji wenzake kuanza maandalizi ya msimu ujao, ambapo watatangaza hapo baadaye wapi watakwenda kuweka kambi.

Alisema msimu ujao wanatarajia kurudi kivingine kutokana na aina ya usajili wanaoufanya ili wairudishe heshima yao.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### ANTONY KUMBADILI RONALDO

KOCHA mpya Erik ten Hag ataiomba Manchester United kumnunua mshambuliaji wa Ajax, Antony, 22, ikiwa fowadi Cristiano Ronaldo, 37, ataruhusiwa kuondoka msimu huu. ***(Mirror Sunday)***

#### MAN YAITIBULIA ARSENAL

KLABU ya Manchester United imevunja matumaini ya Arsenal kwa ajili ya kumnunua Lisandro Martinez, 24, wakiwapatia Ajax dau la pauni milioni 38 ili kumsajili beki huyo wa kati wa Argentina. ***(Mail on Sunday).***

#### GNABRY AGOMBEWA

ARSENAL na Manchester United pia zinapigana vikumbo kumwania winga wa Ujerumani, Serge Gnabry, 26, kutoka Bayern Munich kwa pauni milioni 40. Mchezaji huyo wa zamani wa washikabunduki hao mkataba wake na Bayern unaisha msimu ujao wa joto. ***(Star Sunday)***

#### STERLING KUMPISHA SERGE

SERGE Gnabry atakuwa kileleni mwa orodha ya wachezaji wanaosakwa na Manchester City iwapo watamuuza mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, 27, msimu huu wa joto. ***(Sunday news)***

#### SALAH NUSURU ATUE CHELSEA

MOHAMED Salah, 30, alikuwa tayari kujiunga tena na Chelsea kabla ya mshambuliaji huyo wa Misri kukubali mkataba mpya ambao ulimfanya kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia ya Liverpool. ***(Sunday news)***

#### DE JONG KUKATWA

BARCELONA hawana nia ya kumuuza kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, ingawa wanataka mchezaji huyo anayelengwa na Manchester United, akubali kukatwa mshahara. ***(AS)***

#### TAGLIAFICO KUONDOKA

NICOLAS Tagliafico, 29, anatarajiwa kuondoka Ajax msimu huu wa joto, huku Brighton na Lyon zikiwa miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili beki huyo wa Argentina. ***(Fabrizio Romano, Twitter).***

#### NIAKHATE HUYO FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kumsajili beki wa kati wa Ufaransa, Moussa Niakhate, 26, baada ya kufikia makubaliano kimsingi juu ya ada ya uhamisho na Mainz. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

#### GIBBS-WHITE ATAKIWA

KLABU ya Crystal Palace inapanga kumsajili kiungo wa kati wa Wolves, Morgan Gibbs-White, 22, mwenye thamani ya pauni milioni 20. ***(Sunday Sun).***


#### VERON AWANIWA

MANCHESTER United inafikiria kumnunua winga wa Palmeiras kutoka Brazil, Gabriel Veron, 19, kwa pauni milioni 10. ***(Sunday Mirror).***

#### TELLES KUUZWA

MLINZI wa kushoto wa Brazil, Alex Telles, 29, anatarajiwa kuuzwa na Manchester United baada ya kuhusika katika ugomvi kwenye uwanja wa mazoezi na kiungo wa kati, Hannibal Mejbri, 19. ***(Sunday Mirror).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# RONALDO SASA AOMBA KUONDOKA MAN UNITED

●●● Yadaiwa anataka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Man wenyewe...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo ameiomba Manchester United kumwachia aondoke katika klabu hiyo iwapo watapata ofa bora kwa ajili yake msimu huu wa joto.

> **Mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37, alirejea hapo Old Trafford kutoka Juventus msimu wa joto uliopita.**

Hata hivyo, licha ya kuwa mfungaji bora wa United msimu uliopita na wa tatu katika Ligi Kuu msimu wote kwa jumla ilionekana kuwa sio mzuri zaidi kwake.

United walimaliza katika nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu hivyo wakakosa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hiyo ina maana kwamba Ronaldo, ambaye amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake na United, atacheza katika Ligi ya Europa kwa mara ya kwanza.

Sio kitu anachofurahia na mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or anahisi kunaweza kuwa na chaguo la kuvutia zaidi katika kipindi hiki katika maisha yake ya soka.

Fowadi huyo wa zamani wa Real Madrid ana wasiwasi akisisitiza kuwa anaiheshimu United lakini anapoingia katika hatua za mwisho za maisha yake ya soka, anataka kuwania tuzo kubwa zaidi.

United bado haijasema lolote kuhusu mustakabali wa Ronaldo, ingawa awali vyanzo vya habari viliamini kwamba Mreno huyo angesalia Old Trafford msimu ujao.

Ingawa itakuwa pigo kwa United ikiwa watampoteza mmoja wa wachezaji bora zaidi ambao wamewahi kuwa nao, pia ingesuluhisha masuala machache kwa kocha mpya, Erik ten Hag.

Ingawa Ten Hag amesema anatazamia kuungana na Ronaldo, haijabainika ni kwa namna gani uchezaji wa fowadi huyo utaendana na Mholanzi huyo. Zaidi ya hayo, Ronaldo ndiye mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya England.

Ronaldo anatarajiwa kurejea klabuni hapo kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wiki hii na anatarajiwa atakuwa kwenye ziara yao ya maandalizi ya msimu mpya nchini Thailand na Australia.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 274,

MECHI KALI
TPS TURKU
VERSUS
FC KTP
1 | 1.83
X | 3.44
2 | 3.83

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DEMBELE, BARCA MAMBO MAGUMU




**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ameweka wazi kuhusu sakata la mkataba mpya wa Ousmane Dembele linaloendelea, akisisitiza kuwa mchezaji huyo atasalia tu Camp Nou ikiwa atakubali ofa iliyopo mezani.

Dembele tayari ni mchezaji huru baada ya kumalizika kwa mkataba wake Alhamisi iliyopita na pia alikuwa na nafasi ya kuzungumza rasmi na klabu nyingine kuanzia Januari.

Barcelona walikuwa na nia ya kumuuza Januari, lakini hawakuweza kupata dili kabla ya tarehe ya mwisho ya uhamisho wa wachezaji.

Mfaransa huyo, Februari na Machi, alionekana kubadilisha mambo kuhusiana na mustakabali wake, lakini hakuna makubaliano juu ya mpango mpya yaliyofikiwa.

Chelsea imekuwa ikimfuatilia Dembele na walikuwa wanataka kuzungumza na mchezaji huyo kwa nia ya kupanga uhamisho wa bure.

Lakini Barcelona walianza tena mazungumzo yao ya mkataba mpya mwishoni mwa Juni kwa ombi la kocha mkuu, Xavi.

## 'Tulijua Mbappe anakuja Real'



**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Luka Modric amesisitiza kwamba, Los Blancos wanaheshimu uamuzi wa Kylian Mbappe kusalia kule Paris Saint-Germain, ingawa wachezaji 'wote' walidhani angejiunga nao.

Mbappe alimaliza mkataba wake na PSG na ilionekana kama atahamia Real kama mchezaji huru, lakini wakati ulipofika, aliamua kusaini mkataba mpya na miamba hiyo ya jiji la Paris hadi mwaka 2025.

Rais wa Real Madrid, Florentino Perez alidai ilikuwa 'ndoto' ya Mbappe kujiunga na Los Blancos, lakini alibadili mawazo yake wiki mbili kabla na kuamua kubaki PSG.

"Ndoto yake ilikuwa kucheza Real Madrid, tulitaka kufanya hivyo Agosti iliyopita na hawakumruhusu kuondoka, aliendelea kusema anataka kucheza Madrid na kama siku 15 kabla ya kubadilisha hali hiyo," alisema Perez.

Sasa, akizungumza na Sportske Novosti ya Croatia, Modric amesema, "Mbappe aliamua kama alivyoamua, hiyo ni haki yake na sasa anaishi na uamuzi huo.



002,680

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06.07.22 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Nagoya Grampus | 2.35 | 2.94 | 2.99 |
| 02. 06.07.22 | 13:00 | Renofa Yamaguchi vs Oita Trinita | 3.15 | 3.05 | 2.20 |
| 03. 06.07.22 | 13:00 | Yokohama F Marinos vs Sanfrecce Hiroshima | 2.20 | 3.25 | 2.95 |
| 04. 06.07.22 | 13:00 | Jubilo Iwata vs Avispa Fukuoka | 2.85 | 2.95 | 2.44 |
| 05. 06.07.22 | 13:00 | Vegalta Sendai vs Ventforet Kofu | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 06. 06.07.22 | 13:00 | Incheon Utd vs Suwon City | 2.18 | 3.14 | 3.09 |
| 07. 06.07.22 | 13:00 | Suwon Samsung vs Daegu | 2.56 | 3.15 | 2.56 |
| 08. 06.07.22 | 13:00 | Roasso Kumamoto vs Tokushima Vortis | 2.60 | 2.90 | 2.70 |
| 09. 06.07.22 | 13:00 | V Varen Nagasaki vs Montedio Yamagata | 2.21 | 3.09 | 3.09 |
| 10. 06.07.22 | 13:00 | Jeonnam Dragons vs Gyeongnam | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 11. 06.07.22 | 13:30 | FC Seoul vs Jeonbuk Hyundai | 3.09 | 3.14 | 2.19 |
| 12. 07.07.22 | 19:00 | Grorud IL vs Sandnes Ulf | 2.60 | 3.34 | 2.40 |
| 13. 06.07.22 | 19:00 | Kristiansund vs Tromso | 2.80 | 3.45 | 2.33 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 04/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1748 | Shadhinata Krira Sangha vs Bangladesh Police Club | 4.02 | 3.92 | 1.68 |
| 13:00 | 5231 | Rahmatgonj Mfs vs Muktijoddha Sangsad KC | 1.84 | 3.19 | 4.13 |
| 14:30 | 1806 | Chengdu Qianbao vs Shijiazhuang | 1.66 | 3.49 | 4.72 |
| 14:45 | 3877 | Albirex Niigata (SIN) vs Tampines | 1.46 | 4.71 | 4.91 |
| 15:15 | 4471 | CLB Viettel vs Hong Linh HA Tinh FC | 1.54 | 3.80 | 6.00 |
| 17:00 | 3001 | Ordabasy vs FK Kaspiy Aktau | 2.19 | 3.24 | 2.99 |
| 17:00 | 3243 | Metallurg Bekabad vs Pakhtakor | 5.89 | 3.73 | 1.51 |
| 17:00 | 5629 | Patronato Reserve vs Newells Old Boys | 2.75 | 3.19 | 2.37 |
| 18:00 | 2992 | Hifk vs Ilves Tampere | 3.33 | 3.28 | 2.02 |
| 18:00 | 3028 | Dnepr Mogilev vs FC Minsk | 4.02 | 3.58 | 1.75 |
| 18:00 | 4365 | Nasaf Qarshi vs Surkhon Termez | 1.30 | 4.71 | 8.64 |
| 18:30 | 1832 | Honefoss vs Aalesund 2 | 2.33 | 4.02 | 2.36 |
| 18:30 | 2167 | TPS Turku vs FC KTP | 1.83 | 3.44 | 3.83 |
| 18:30 | 5289 | Musa Pori vs Klubi 04 | 3.39 | 3.83 | 1.84 |
| 19:00 | 1155 | FC Elva vs FC Nomme United | 2.15 | 3.79 | 2.93 |
| 19:00 | 2235 | Fredrikstad vs Aasane Fotball | 1.54 | 4.12 | 4.81 |
| 19:00 | 2348 | Harju JK Laagri vs Paide Linnameeskond | 1.18 | 7.47 | 11.11 |
| 19:00 | 2887 | Stjordals vs Blink-IK Start | 4.41 | 4.11 | 1.59 |
| 19:00 | 3854 | Kongsvinger IL vs Ranheim | 2.50 | 3.52 | 2.41 |
| 19:00 | 4436 | Viking FK 2 vs Brodd | 2.30 | 3.92 | 2.44 |
| 19:00 | 4859 | Flora II vs Viljandi Tulevik | 1.11 | 8.87 | 18.14 |
| 19:00 | 4988 | Brann vs Bryne | 1.14 | 6.84 | 12.70 |
| 19:00 | 5302 | Sandnes Ulf vs Raufoss | 1.98 | 3.57 | 3.18 |
| 19:00 | 5706 | Ida-Virumaa FC Alliance vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.80 | 3.89 | 3.89 |
| 19:30 | 3195 | Hodd 2 vs Molde FK 2 | 5.29 | 5.09 | 1.40 |
| 20:00 | 1093 | Olympique Safi vs CRS Salmi | 1.37 | 4.33 | 7.28 |
| 20:00 | 1329 | IFK Goteborg vs Degerfors | 1.59 | 3.82 | 4.80 |
| 20:00 | 3232 | CSKA Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.50 | 4.22 | 5.10 |
| 20:00 | 3966 | Athletic Youssoufia vs RS Berkane | 5.11 | 3.34 | 1.65 |
| 20:00 | 4283 | Torpedo Zhodino vs Slutsk | 1.94 | 3.24 | 3.64 |
| 20:00 | 4631 | Wydad Casablanca vs FUS Rabat | 1.64 | 3.54 | 4.81 |
| 20:00 | 5192 | Trelleborgs FF vs Norrby IF | 2.48 | 3.26 | 2.86 |
| 20:00 | 5744 | Nigeria W vs South Africa W | 2.09 | 3.08 | 3.38 |
| 20:30 | 5899 | Pachuca U20 vs Queretaro U20 | 1.56 | 3.95 | 5.40 |
| 21:00 | 1324 | KA Akureyri vs Valur | 2.65 | 3.44 | 2.31 |
| 21:00 | 3476 | EC Prospera SC vs GE Juventus SC | 2.66 | 2.66 | 2.86 |
| 21:00 | 5439 | Gimnasia Jujuy vs Deportivo Madryn | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 21:00 | 5597 | Villa Dalmine vs Atletico Alvarado | 2.22 | 2.80 | 3.43 |
| 21:30 | 4477 | General Lamadrid vs Argentino Merlo | 2.60 | 2.80 | 2.80 |
| 21:30 | 5607 | Deportivo Espanol vs Excursionistas | 2.66 | 2.71 | 2.81 |
| 22:15 | 1188 | Hafnarfjordur vs Stjarnan | 1.99 | 3.63 | 3.09 |
| 22:15 | 3707 | Leiknir vs IA Akranes | 1.99 | 3.58 | 3.14 |
| 22:15 | 4771 | IR Reykjavik vs Aegir | 1.95 | 4.02 | 2.94 |
| 23:00 | 5105 | Arsenal Sarandi vs Estudiantes LP | 2.40 | 3.05 | 2.81 |

JUMANNE - 05/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 1159 | Aldosivi vs Rosario Central | 3.05 | 3.15 | 2.20 |
| 01:00 | 3238 | San Luis Quillota vs Cobreloa | 2.70 | 3.14 | 2.43 |
| 01:00 | 5432 | NewellS Old Boys vs Patronato Parana | 1.92 | 3.13 | 3.86 |
| 02:00 | 2877 | Orlando City vs DC United | 1.90 | 3.68 | 3.83 |
| 02:00 | 5372 | Bragantino SP vs Botafogo RJ | 1.66 | 3.39 | 4.92 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# GEOFREY WA YANGA ATUA SINGIDA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Paul Geofrey, amejiunga na klabu ya Singida Big Stars kwa mkataba wa miaka miwili, ikiwa ni siku moja tu baada ya klabu hiyo kumtambulisha mchezaji wa Mbeya City, Aziz Andambile.

Taarifa ya klabu hiyo jana imesema kuwa imemsajili mchezaji huyo kutoka kwenye klabu ya Yanga, huku ikiweka picha ya mchezaji huyo kwenye mtandao rasmi wa klabu yao, akiwa pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu, Muhibu Kanu.

**Geofrey ambaye ameichezea Yanga kwa misimu kadhaa ameamua kuondoka kwenda kutafuta changamoto nyingine, baada ya kuwepo ushindani wa namba za pembeni kwenye klabu hiyo ambayo kwa sasa ni Mabingwa wa Tanzania Bara na Kombe la FA.**

Singida Big Stars, klabu ambayo imepanda daraja kwa jina la DTB na kutarajia kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu ujao, imeanza zoezi la usajili kwa kasi kubwa, kwani kabla ya kumsajili mchezaji hiyo, ilikuwa imemtambulisha kiungo mkabaji wa Mbeya City na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars Andambwile.

Kiungo huyo alikuwa pia akiwaniwa na klabu kadhaa kubwa na hasa Azam FC ambayo ilionekana kuwa inamhitaji zaidi, kabla ya timu hiyo kuingilia dili hilo.

Kabla ya usajili huo, ilikuwa imemsainisha straika wa Mbeya Kwanza, Habib Kyombo.




Kamishna wa mchezo wa fainali ya Kombe la FA, Somoe Ng'itu (watatu kushoto) akiwa na waamuzi na mtathmini wa waamuzi, Nassor Hamduni kutoka Kigoma pamoja baada ya fainali hiyo. Yanga ilitwaa ubingwa baada ya kuifunga Coastal Union penalti 4-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# *Tariq ataka Polisi kusajili*

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Polisi Tanzania, Tariq Seif ameuomba uongozi wa timu hiyo kulitumia vyema dirisha kubwa la usajili ili msimu ujao waweze kuwa na timu itakayopigania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mshambuliaji huyo ameeleza kuwa kilichowakwamisha msimu huu hata wakashindwa kupigania ubingwa ni madhaifu yaliyokuwapo kwenye kikosi chao ukilinganisha na timu nyingine kama za Yanga, Simba na Azam FC.

"Ninachoamini kama tutafanya usajili mzuri uwezekano wa Polisi kupigania ubingwa msimu ujao ni mkubwa kutokana na uwazi uliokuwapo kwenye ligi yetu hivi sasa tofauti na huko nyuma ambapo timu za Simba na Yanga pekee ndio zilikuwa zinaangaliwa," amesema Seif.

Mshambuliaji huyo aliyewahi kuzichezea klabu za Biashara United na Yanga amesema kama uzoefu kwenye ligi wameshaupata kinachotakiwa kwa sasa ni kubeba mataji ili kuingia kwenye rekodi.

# Michezo

Jumatatu Julai 4, 2022

Nipashe




Ronaldo aomba kuondoka Utd UKURASA 21



Abdul Selemani 'Sopu' akipokea tuzo ya mchezaji bora wa mchezo wa fainali ya kombe la FA kati ya timu yake na Yanga, uliopigwa uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Jumamosi. **PICHA: TFF**

# Sopu aziingiza vitani Simba, Yanga, Azam

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Zote zawania saini yake baada kuupiga mwingi FA, Azam watajwa kuweka mzigo mkubwa...

BAADA ya kuonyesha kiwango cha hali ya juu kwenye mechi dhidi ya Yanga, akifunga mabao matatu 'hat-trick' katika fainali ya Kombe la FA, Jumamosi Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, klabu za Simba, Yanga na Azam zimeingia vitani kuwania saini ya Abdul Selemani 'Sopu'.

**Habari zinasema kuwa Simba ambayo awali ilikuwa ina uhakika wa kumsajili mchezaji huyo kwa sababu alitokea kwenye kikosi chao cha pili, kabla ya kupandishwa na kupelekwa kwa mkopo Ndanda FC, na baadaye kutua Coastal Union, kwa sasa inakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Yanga na Azam ambazo nazo zinaonekana kuingilia dili hilo.**

Wakati kiungo wa Coastal, Mnigeria, Victor Akpan mwenyewe akisema ilikuwa ni mechi yake ya mwisho, huku akiripotiwa kuwa kwenye hatua za mwisho za kumalizana na Simba, Sopu amekuwa na kigugumizi ni wapi atakwenda msimu ujao baada ya kumaliza mkataba wake na Coastal Union.

"Ni kweli Simba wananihitaji, lakini siyo wao peke yao tu, ni timu nyingi na mpira ndiyo kazi yangu, ila kwa sasa siwezi kuelezea mambo ya mkataba wangu na wapi naelekea," alisema winga huyo ambaye kwa sasa anachezeshwa pia kama mshambuliaji wa kati.

Kuhusu kuongea na Kaimu Ofisa Mkuu wa Yanga, Senzo Mazingiza baada ya mechi hiyo, ikihusishwa kumshawishi kujiunga na klabu hiyo, alikataa na kusema kuwa alichokuwa akipewa ni pongezi tu.

"Senzo alichokuwa akiniambia ni kunipongeza tu na hakuna chochote kilichokuwa kikiendelea," alisema.

Hata hivyo, tetesi zinasema kuwa mchezaji huyo anatamani kurejea kwenye klabu yake ya Simba, lakini tayari Azam imeweka mzigo mkubwa zaidi ambazo zinawatoa udenda watu wanaomzunguka na kumshawishi kwenda huko.

Kwenye mtandao wa Instagram, shabiki mmoja wa Azam alimwandikia mmiliki wa klabu ya Azam FC, Yusuph Bakhresa kuwa wanamhitaji kwa udi na uvumba mchezaji huyo, hivyo akimtaka kufanya jambo kama alivyofanya kwa kina Issa Ndala.

Sopu, ndiye aliyeiokoa Coastal Union kutoshuka daraja msimu uliopita kwenye 'play off'.

# Manara kikaangoni TFF

**Na Mwandishi Wetu**

MSEMAJI wa Yanga, Haji Manara ameripotiwa kufunguliwa shauri mbele ya kamati ya maadili iliyochini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kutokana na kile ambacho kilitokea Jumamosi kwenye mchezo wa fainali ya FA.

Awali ilionekana juzi kwenye video fupi iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii kutokea Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, ofisa huyo wa Yanga ni kama akitupiana maneno na Rais wa TFF, Wallace Karia.

Lakini baada ya mchezo wa fainali ambayo Yanga ilitwaa taji lao la tatu msimu huu, Manara alitumia ukurasa wake wa Instagram kueleza juu ya kile ambacho kilitokea huku akikanusha madai ya kumtukana rais huyo kama ilivyokuwa ikielezwa kwenye mitandao ya kijamii.



Jana, Jumapili TFF ilitoa taarifa ya kwamba Sekretarieti yake imefungua shauri mbele ya Kamati ya Maadili dhidi ya ofisa huyo ambaye aliwahi kuhudumu kwenye klabu ya Simba.

Taarifa iliyotolewa jana na TFF, kupitia kwa Ofisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo, ilimesema kuwa kamati hiyo kupitia mwenyekiti wake tayari imepewa taarifa kuhusu malalamiko dhidi ya Manara, hivyo itapanga siku ya kusikiliza shauri hilo na mlalamikiwa atapewa taarifa.

Taarifa hiyo ilieleza kwamba, "Kamati ya maadili kupitia kwa Mwenyekiti wake, tayari imepewa taarifa kuhusu malalamiko dhidi ya Manara, hivyo itapanga siku ya kusikiliza shauri hilo na malalamikiwa atapewa taarifa."

Iliongeza; "TFF inawakumbusha wanafamilia ya mpira wa miguu kuwa wanabanwa na katiba na kanuni mbalimbali za mchezo huo, hivyo wanatakiwa kuwa makini kwa vitendo na kauli zao kuhusu mpira wa miguu."

9 770856 541002 >